ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg Yahya Khamis Hamad	**Kny: Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Sita – Tarehe 25 Januari, 2012

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Waziri Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha ripoti ya Tume ya Haki za Binaadam na Utawala Bora kwa kipindi cha mwaka 2007/2008

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu Kny Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka Mezani hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kuhusu taarifa ya Waziri juu ya Taarifa ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora kwa Upande wa Zanzibar ya Mwaka 2007/2008.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 70

Ofisi za Kibalozi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza :-

Tanzania ina sifa ya kuwa na urafiki na nchi nyingi ulimwenguni na kusababisha kuwa na Ofisi nyingi za Kibalozi katika nchi mbali mbali.

(a) Je, Tanzania ina Ofisi ngapi za Kibalozi ulimwenguni.
(b) Je, Mabalozi wangapi ni Wazanzibari kati ya mabalozi wanaotumikia Ofisi zetu za Kibalozi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu :-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 70 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kikao cha nne cha Baraza la Wawakilishi wakati wa kipindi cha masuala na majibu nilijibu suala namba. 200 ambalo lilifanana na suala hili la Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

a) Mhe. Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazo ofisi za Kibalozi thalathini na mbili (32) na ofisi ndogo za Kibalozi (*Consulates*) mbili (2). Pia inazo Balozi mbali mbali za heshima yaani *"Honorary Consulates"* katika baadhi ya nchi duniani.

b) Mhe. Mwenyekiti, Ofisi za Kibalozi zinaongozwa na Wazanzibari ni tatu ambazo ni:-

- *Stock holm* – Sweden, Balozi Mohamed Mzale,
- Cairo – Misri Balozi Moh'd Haji Hamza
- Mascat – Oman Balozi Ali Saleh

Aidha Balozi Ramadhani Muombwa Mwinyi ameteuliwa kuwa Balozi mdogo wa kudumu katika Umoja wa Mataifa huo New Yourk na Balozii Mdogo Yahya Jemba huko Mombasa Kenya. Balozi Omar Ramadhan Mapuri na Ali Shauri ambao walikuwa China na Misri watarejea nchini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mhe. Waziri naomba nimuulize masuala mawili madogo.

(a) Ni vigezo gani vinavyotumika kabla ya uteuzi wa Mabalozi wanaotoka Zanzibar kabla ya kuteuliwa.

(b) Idadi uliyoieleza ya Mabalozi je, kuna Wazanzibari wangapi wamenufaika katika nafasi zao za utendaji katika Afisi za ubalozi wa Tanzania kutoka Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Kuhusu vigezo zipo taratibu zinazofuata mpaka kufikia kuwa Balozi na hivyo ni utaratibu wa kawaida ipo pale Wizara ya Mambo ya nchih za nje. Lakini kuhusu uteuzi wa kuwa balozi wa kupelekwa katika nchi mbali mbali duniani, hiyo upo kwenye uwezo wa Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Kuhusu watendaji ni kweli hakuna uwiyano wa kutosha kati ya watendaji kutoka Zanzibar na wale wanaotoka upande wa Tanzania Bara. Ndio maana jambo hili likawa

ni moja katika kero za Muungano. Hivi sasa linashughulikiwa ili Wazanzibari wapate kota yao ndani ya taasisi za Muungano. Kwa hivyo namuomba Mhe. Jaku aendelee kuvuta subirá kwa kuwa hili jambo lipo katika hatua za mwisho kumalizika ili Wazanzibari na wao wapate nafasi hizi kwa uwiyano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Kwanza nadhani Mhe. Waziri akubaliane na sisi kwamba sio kwamba hakuna uwiyano kidogo, hakuna uwiyano kabisa baina ya Zanzibar na Bara. Lakini naomba niulize suala la ngu la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar ambaye alikuwa mjumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa muda mrefu sana Mhe. Hassan Nassoro Moyo amewahi kunukuliwa akisema kwamba katika kipindi cha mwaka 1971 mwishoni, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa aliyekuwa raisi wa Kwanza kabisa, Mhe. Mzee Abeid Amani Karume. Ilipeleka pendekezo la kutaka nafasi hizi katika Utumishi wa Mambo ya Nje baina ya Zanzibar na Tanganyika zigaiwe nusu kwa nunu ili kuuweka msingi wa muungano huu kwamba ni wa nchi mbili zilizohuru na sawa.

Je, serikali hivi sasa ya awaumu ya saba yenye muundo wa Umoja wa Kimataifa ipo tayari kusimamia pendekezo hilo la Mzee Karume, ili kuona sasa baada ya miaka zaidi ya 30 lilipowasilishwa linatekelezwa na Zanzibar inapata haki zake katika mabalozi na maafisa wa kibalozi katika Balozi zilizokuwepo katika nchi za Nje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, wazo ni zuri na ndio maana sisi katika serikali tumeona kwamba upo umuhimu wa Zanzibar kupata haki yao

katika tasisi za Muungano. Ndio maana jambo hili tunalizungumza ili kuwepo na uwiyano.

Ushauri wa ndugu yangu Mhe. Jussa tunauchukua, tutaufanyia kazi ili haki za Wazanzibari ziweze kulindwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kuuliza suali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza suali lifuatalo.

Kwa kuwa historia ya Zanzibar inaonesha kwamba wanauzoefu mkubwa wa kutoa wana dilomasia tangu mwaka 1964 mpaka leo hii, wamekuwa wanauzoefu wakutoa wana diplomasia wazuri akiwemo Salim Ahmed Salim ambaye ni Mzanzibar. Je, kuendelea kujibu tu kwamba tumo mbioni, kudai haki zetu katika vyombo vya muungano. Haoni Mhe. Waziri anawavunja moyo hawa vijana wetu wa Zanzibar kuingia katika fani hii ya diplomasia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nina furaha kumjibu muasisi mwenzangu wa Mapinduzi Mhe. Saleh kama ifuatavyo. Ni kweli kadiri tunapochelewa kupata ufumbuzi wa matatizo yetu yanayohusiana na masuala ya muungano, sio tu yanavunja moyo kwa sekta nyengine kuchukua nafasi yake vizuri lakini hata wananchi wetu wanavunjika moyo sana. Ni wajibu wetu kuchukua kila hatua kuhakikisha kwamba mambo tunayoyazungumza tunayamaliza na tutayatekeleza.

Nataka nichukua nafasi hii kulihakikishia Baraza lako tukufu na wananchi wote wa Zanzibar kwamba tumekuja na kasi mpya ya kuhakikisha kwamba yale tutakayoyafikia tutayatekeleza.

Nam. 44

Kuuzwa Kwa Viwanda vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza:-

Hapa Zanzibar kulikuwa na viwanda vingi vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na vilisaidia sana kutoa ajira kwa wananchi wetu, lakini sasa inaonyesha ama vimeuzwa au kukodishwa.

(a) Je, viwanda hivyo vilikuwa vingapi.

(b) Je, ni viwanda vingapi bado hadi sasa vinamilikiwa na Serikali.

(c) Je, Taifa letu limepata manufaa gani kuuza viwanda hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 44 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenye, Idadi ya viwanda vilivyokuwa vikimilikiwa na serikali tokea 1964 ilikuwa inabadilika kutokana na kujengwa viwanda vipya katika miaka mbalimbali, kabla serikali haijaanza kujitoa katika umiliki na uendeshaji wa viwanda katika mwaka wa 1993 ilikuwa inamilikiwa jumla ya viwanda 38.

(b) Serikali ilipojiondoa katika umiliki na uendeshaji wa viwanda ilifanya hivyo ama kuuza mitambo ya kiwanda na kuendelea na umiliki wa majengo au kuingia ubia na wawekezaji binafsi katika uendeshaji wa kiwanda na kuuza mitambo na majengo ya kiwanda. Kwa mtizamo

huo nilioutaja hapo juu hivi sasa serikali inamiliki majengo yote ya viwanda ndani ya eneo la viwanda vidogo vidogo (*Amaan Industrial Park)*, pamoja na kuwa na ubia katika mradi wa mafuta ya kula *(Edible Oil Ltd,)* ulio ndani ya eneo hilo. Serikali pia ni mbia katika mradi wa kiwanda cha Chakula cha Mifugo, Maruhubi. Pia Serikali inamiliki moja kwa moja Kiwanda cha Sigara na Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo Wawi Pemba.

(c) Wakati Serikali ilipoamua kujitoa katika uendeshaji wa viwanda katika miaka ya 1980 na 1990, takriban viwanda vyote vilikuwa vikiendeshwa kwa hasara kubwa kwa kuzalisha chini ya uwezo, kuajiri vatu wengi zaidi ya mahitaji na hivyo kutegemea ruzuku kutoka serikalini kwa ajili ya gharama za mishahara na uendeshaji. Kufuatia ubinafsishaji, manufaa yafuatayo yamepatikana.

Serikali imeondokana na jukumu la kulipa mishahara na gharama za uendeshaji zisizo za lazima. Pia serikali inakusanya kodi zinazotokana na bidhaa zinazozalishwa viwandani pamoja na kodi ya majengo yaliyokodishwa kwa wawekezaji binafsi, Teknolojia na mbinu mpya za uzalishaji zinatumika kwa wawekezaji binafsi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize suala la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Mwenyekiti, wataalamu wanatwambia ili uchumi wetu uweze kuchanyuka ni lazima sekta ya viwanda iimarishwe katika nchi yetu. Sasa kwa kuwa Mhe. Waziri alikiri kwamba tulikuwa tunavyo viwanda na hadi sasa majengo haya ya viwanda yanamilikiwa na serikali.

(a) Serikali kwa sasa ina mpango gani ulio hai wa kuvifufua viwanda hivyo pamoja na kuanzisha vyengine vipya.

(b) Kwa kuwa alitwambia kwamba viwanda vilivyoanzishwa vilijiendesha kwa hasara. Je ni sababu zipi zilizopelekea serikali kuanzisha viwanda halafu viiwanda hivyo vikajiendesha kwa hasara.

(c) Iwapo serikali itavifufua na kuanzisha vyengine vipya, serikali itabuni mpango gani ili viwanda hivyo vipya na vitakavyofufuliwa visijiendeshe kwa hasara kama vile vilivyokuwepo awali.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa serikali inao mpango wa kufufua pamoja na kuanzisha viwanda vipya kulingana na rasilimali ambazo zipo nchini, mpango huu utakuwa ni endelevu kwa sababu sasa hivi serikali kupitia wizara tayari inafanya tathmini *feasibility study* ya kuangalia ni viwanda vipi vinavyoweza kukufufuliwa kufuatana na mahitaji ya nchi lakini kufuatana na rasilimali zilizopo. Lakini pia ni viwanda gani ambapo pengine tukianzisha vitaweza kuwa endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi, pia alitaka kujua sababu zilizopelekea kuendesha viwanda vile kwa hasara. Nilisema kwamba itakuwa ni elimu ndogo tuliyokuwanayo baada ya kurithi viwanda vile. Lakini pia ajira kubwa iliyotumika kwenye kuwaajiri wananchi kwenye kuendesha viwanda vile ilipelekea gharama za uendeshaji ziwe kubwa kuliko mapato halisi.

Lakini mkakati Mhe. Mwenyekiti, ambao utatumika unategemea *feasibility* study hii itakavyoelekeza ambayo inafanyiwa kazi na wataalam.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza lenye vifungu (a),(b) na (c) kama hivi ifuatvyo.

Kwa kuwa tuliuliza nyuma, kuhusu mnasaba wa uzalishaji wa chumvi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na ambayo ni bidhaa kubwa tuliyonayo, tukiachilia mbali viwanda vya maji vilivyokuwepo.

(a) Ni sababu zipi zilizozorotesha mpaka hivi leo ikawa bado hakujapatikana uzalishaji wa chumvi hiyo na kusafirishwa.

(b) Kuna uwekezaji mwingi Zanzibar lakini mwingi unaelekezwa katika hoteli za kitalii. Je ni sababu zipi zinazozorotesha uwekezaji katika viwanda uwe ni mdogo sana.

(c) Sheria zinazotawala hususan TRA na mambo ya muungano yanachangia au hayachangii katika kuzorotesha uwekezaji wa viwanda Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, uzalishaji wa chumvi Zanzibar unafanyika lakini utaalamu unaotumika katika uzalishaji chumvi bado haujakidhi matakwa yanayostahiki katika chumvi kuingia katika soko la kimataifa. Kuna kiwanda cha chumvi pale Wawi Pemba, lakini kiwanda kile utakuta ukaushaji wake wa ile chumvi bado haujafikia viwango vinavyotakiwa. Chumvi imabakia bado inakuwa na maji maji, haiwi kavu kama vile inavyotakiwa. Kwa hivyo bado tunasema ni utaalamu mdogo tulionao, lakini tumo kwenye kujifunza na tunasubiri ripoti hii ya wataalamu ili iweze kuelekeza ni vipi tutaweza kujikita zaidi katika sekta hii ya viwanda kulingana na rasilimali tulizonazo.

Pia Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Seif alitaka kujua sababu ambazo zinazorotesha uwekezaji kwenye viwanda. Tumesema ni utaalamu mdogo tulionao. Kwa hivyo ndio maana tukasema kwanza tutafute *feasibility study* ili tujue hasa, tukianza kuekeza

katika sekta ya viwanda tuende vipi tuweze kupata mafanikio tusije tukaachia kati kati kama huko nyuma.

Lakini suala la TRA na muungano kwamba vimechangia kuzorotesha suala zima la viwanda hili siwezi kusema wacha tusubiri *feasibility study* hiyo itakavyoelekeza kwa nini nyuma tulifeli na sasa tunatakiwa tuende vipi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri suala la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili liliwahi kuwaambiwa kwamba Zanzibar ina orodha kubwa ya viwanda vidogo vidogo vikiwemo viwanda vya kutengeneza vidani na chapati. Juzi Mhe. Waziri katika semina yetu ya Afrika Mshariki tuliambiwa kwamba Waziri wetu ni kiongozi wa shughuli za kibiashara Afrika Mashariki.

Je, viwanda hivi vya kutengeneza vidani na chapati, ndivyo ambavyo vinakusudiwa kuingia katika soko la ushindani la Afrika Mashariki.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kuna sababu nyingi sana ambazo zinapelekea kusema kwamba sasa tupo tayari kuanzisha viwanda. Zaidi ni rasilimali tuliyonayo. Utengenezaji wa chapati unatokana na rasilimali nyingi ukiwemo unga wa ngano. Ngano tunaiagiza kutoka Nje. Kwa hiyo namuomba Mhe. Mwakilishi, tuendelee kusubiti ripoti hii itatuelekeza vipi ili tuweze kuanzisha viwanda endelevu.

Nam. 104

Usafirishaji wa Sukari Nje ya Nchi

Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Aliuliza:-

Zanzibar ilikuwa na Kiwanda cha Sukari ambacho kilikuwa kinakidhi haja kiasi fulani. Lakini pia kwa kipindi kirefu tunalazimika kuagiza sukari kutoka nje na mpaka hivi sasa hatuna tatizo la upatikanaji wa sukari. Lakini kumejitokeza usafirishaji wa sukari kwenda nchi jirani kutoka Pemba kwenda Kenya jambo ambalo linaweza kuleta usumbufu mkubwa wa bidhaa hiyo nchini.

(a) Je, Serikali hawalitambui tatizo hili.

(b) Kama Serikali inafahamu tatizo hilo na kuliruhusu haioni kwamba biashara hii ikishamiri sana katika Kisiwa chetu itakuwa ni tatizo hasa kwa vile Zanzibar si wazalishaji wa sukari.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 104 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilikuwa hatutambua tatizo la magondo ya sukari, lakini kwa vile tumepata tarifa ya kuwepo kwa jambo hilo. Wizara kwa kushirikiana na taasisi husika tutalichukua suala hilo kwa kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya kuchukua tahadhari ya kutokea tatizo kama hilo, serikali tayari imeshapiga marufuku kwa sheria yake Nam. 4 ya mwaka 1986/88 ya usafirishaji wa bidhaa hasa za chakula kutoka nje ya Zanzibar. Ila kwa wale wanaofanya biashara wanaosafirisha bidhaa kutoka Unguja kwenda Pemba

huruhusiwa kwa vibali maalum ambavyo vinatolewa kwa utaratibu maalum na kuhakikisha bidhaa hizo kweli zinafika Pemba na si vyenginevyo.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini nataka nimuulize suala la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Wazili alisema kwamba serikali ilikuwa haina taarifa ya usafirishaji wa sukari hii.

(a) Je, tarifa hiyo waliipata na vikosi ambavyo vimewekwa kama ni walinzi KMKM?

(b) Dhamira ya Mapinduzi ya Kilimo ya Miaka ijayo ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini ni kutekeleza mkakati wa kuanzishwa hakiba ya chakula Zanzibar. Je, Mhe. Waziri huo kuwa usafirishaji huo wa sukari utakapoendelea dhamira hii itaondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Nimesema kwamba taarifa ya kusafirisha sukari kutoka Zanzibar kwenda nje ya Zanzibar tulikuwa hatuna. Tumeipata tarifa hiyo kufuatia suala lake alilotuuliza. Tokea tumepata taarifa hiyo kupitia suala lake ndio tunalifanyia kazi pamoja na taasisi husika vikiwemo hivyo vikosi alivyovitaja Mhe. Bikame.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuanzisha ghala au hakiba ya chakula. Na kufuatia dhamira hiyo naomba nimkumbushe Mhe. Bikame kwamba tayari sheria ilishawasilishwa hapa na Wizara husika ambayo ni Wizara ya Kilimo na Maliasili. Sasa namuomba Mheshimiwa arejee

katika hansard za wizara aone ni kiasi gani serikali imedhamiria kuanzisha jambo hilo. Na michango mizuri sana iliyotolewa na Wawakilishi ndani ya Baraza hili tukufu katika kuweka vyema sheria hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa mara nyengine tena ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika suala mama kumezungumziwa kuwepo kwa Kiwanda cha Sukari hapa Zanzibar ambacho muulizaji anasema kilikuwa kinakidhi haja kwa kiasi fulani, kiwanda hiki tuliwahi kuripotiwa kwamba kilibinafsishwa au kilitolewa kwa mwekezaji fulani. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba taarifa zilizokuwepo ni kwamba mwekezaji aliyepewa kiwanda hiki amekuwa hakitumii tena kwa kuzalisha sukari, lakini badala yake alikuwa anakitumia kuzalisha bidhaa fulani inayotumika katika kutengeneza pombe na kuisafirisha nje ya Zanzibar katika viwanda vilivyokuwepo Ulaya. Mhe. Mwenyekiti, sijui baada ya hatua hii serikali kwanza inaweza kuthibitisha kwamba hivyo ndivyo anavyofanya mwekezaji na ikiwa ni hivyo inachukua hatua gani ili kukirejesha kiwanda hiki katika mikono ya serikali na kutafuta mwekezaji mwenye maana ambaye atatusaidia kuzalisha sukari badala ya kuzalisha bidhaa zinazotumika kutengenezea pombe.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Kiwanda cha Sukari kimekuwa kinaendeshwa kwa kuzalisha sio sukari lakini ni *spirit* na hili serikali inalitambua na kwa kulitambua hili ndipo serikali imeunda kamati maalum ya mawaziri na viongozi wengine ngazi za Mikoa ili kulifuatilia na hatimae kuwasilisha taarifa rasmi serikalini. Kwa hivyo, tunakiri kwamba kweli hazalishi sukari lakini anazalisha *spirit*.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la

nyongeza. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la Mhe. Mwakilishi amekiri kama mwekezaji huyu aliyepewa kiwanda hicho alitiliana mkataba na serikali kwa ajili ya kuzalisha sukari, lakini kinyume chake mwekezaji huyu anazalisha *spirit*.

Je, Mhe. Naibu Waziri kwanza haoni kama mwekezaji huyu amevunja mkataba waliotiliana saini na serikali. Na je kama amevunja mkataba kuna haja gani ya kuundwa kamati tena na wakati yeye ameshavunja mkataba achukuliwe hatua za kinidhamu zinazofaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kweli kwa mtazamo tunaona kwamba amevunja mkataba, lakini hili suala lina umuhimu wake kufuatilia ili tuweze kujua hasa ni sababu zipi zilizopelekea azalishe *spirit* na sio sukari.

Pia namuomba Mhe. Mwakilishi kwamba pamoja na adhma nzuri ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini bado taratibu hazina budi kufuatwa katika shughuli zake. Na kwa kulibaini hilo lazima tuheshimu maamuzi ya serikali wamekaa wakalizingatia ya juu ya mawaziri na kwa hiyo wakaona ni vyema pawe na pakuanzia ndio wakaanzia kwa kuunda kamati hii yenye viongozi mahiri na wenye uzoefu wakishirikiana na viongozi wa Mkoa wa Kaskazini ili hatimae tuweze kujua lazima na sisi tuwe na hatua za kuchukua. Kwa hivyo, hatuwezi kuchukua hatua kama halitofuatiliwa kwa kina tuweze kujua tunalifanyia kazi vipi na kwa kiwango gani.

Nam. 67

Uwezeshaji wa Wanawake

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali inajua wazi kuwa kumuwezesha mwanamke ni sawa na kuiwezesha jamii.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe.Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kumwezesha mwanamke ni sawa na kuiwezesha jamii. Kwa kulijua hilo wizara imekua ikichukua juhudi kubwa za kuwawezesha wanawake hasa kiuchumi ili waweze kujiinua kimaisha. Miongoni mwa juhudi hizo ni kuwapatia ushauri na mafunzo ili kuvikuza vikundi vyao.

   Kwa upande wa mikopo, wizara yangu kwa hivi sasa haitoi mikopo isipokuwa inawahamasisha na kuwaelekeza wanawake kupitia vikundi vyao kujiunga na taasisi mbali mbali zinazotoa mikopo hapa nchini.

   Aidha, wizara huwasisitiza wanawake hao kuitumia mikopo hiyo kwa lengo lilokusudiwa na kuirejesha mikopo kwa wakati.

   Mhe. Mwenyekiti, naomba vile vile kutoa taarifa kwamba wizara yangu hivi sasa tayari imeshaanzisha na kuzindua rasmi *SACCOS* ya Konde na pia wizara iko mbioni kuzindua *SACCOS* ya Mkoani Pemba na kuzindua *SACCOS* ya Tumbe na itafuatiwa na *SACCOS* ya Micheweni kwa upande wa Pemba na hatimae lengo ni kuwa na *SACCOS Bank* katika kila Wilaya za Unguja na Pemba ili kuwarahisishia wanawake kupata mikopo ya kiuchumi na kuendeleza shughuli zao za kujiongezea kipato na kuondosha umasikini.

Aidha, wizara imekuwa ikiwasaidia kuwaunganisha wanawake wafanyabiashara katika maonesho ya kibiashara mfano, maonesho ya sabasaba na maonesho ya juakali nguvu kazi ya Afrika Mashariki. Lengo ni kuwawezesha wanawake kupata masoko ya bidhaa zao na kujifunza kutoka kwa wafanya biashara wa maeneo mengine.

b) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haijawagawa wanawake katka kada hasa katika msuala ya kuwaendeleza kiuchumi, wanawake wote katika vikundi vyao ni sawa sawa na wanapata fursa sawa ya kuendelezwa kinachozingatiwa zaidi ni jinsi kikundi kilivyoundwa, kinavyojituma kwa kutumia mafunzo waliyopata, mpangilio mzuri wa miradi na uendeshaji na jinsi wanavyorejesha mikopo yao kwa wakati na kufuata vizuri masharti waliyopewa hayo ndio mambo muhimu yanayozingatiwa zaidi katika kupata mikopo ili kuharasisha maendeleo yao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tangu kuanzishwa mfumo wa *SACCOS* wananchi wengi wameonekana kuhamasika ingawa tatizo kubwa ni upungufu wa mitaji na kukosekana kwa ujuzi.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo hasa viongozi wa *SACCOS* hizo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, serikali iko mbioni sana na inawasaidia sana wanawake katika kupata misaada mbali mbali. Vile vile kuna *SACCOS* mbali mbali zimeundwa kwa ajili ya wenzetu hawa kupata mikopo kwa mfano kuna *SACCOS* za *Pride*, kuna *SACCOS* za wajasiri amali wanawake wa Zanzibar,

kuna *NGOs* zinazojitosheleza kwa wafanyakazi kwa kutoa mikopo kupitia *SACCOS* zao, kuna mfuko unaotoa mikopo wafanyabiashara wanawake na wanaume, kuna mifuko mbali mbali inayojitegemea, kuna Mfuko wa AK na JK ilimradi wenzetu waweze kupata mikopo mbali mbali.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwa kuwa amekiri kwamba Serikali yetu ya awamu ya saba iko mbioni muda wote kuwatendea haki wananchi, lakini je serikali ina mpango gani wa kufungua benki za wanawake ili kuimarisha hali zao za kiuchumi na kupunguza mbio za serikali.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, serikali ina mpango mzuri sana wa kufungua benki za wanawake, lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba nikwambie kwamba katika kufungua hizi benki hatuwezi kuwaweka peke yao wanawake lazima kutakuwa kuna mchanganyiko kidogo.

Lakini sasa hivi tunazo benki kwa mfano hivi juzi tu kule konde ilizinduliwa benki ambayo ina mchanganyiko baina ya wanawake na wanaume ambayo benki hiyo wao wana mpango mzuri sana wakuwasaidia wanawake na kuwasaidia hata wanaume ilimradi wanawake wajue kwamba wana sehemu zao za kupatia mikopo. Vile vile tutafungua benki Mkoani, tutafungua benki za wanawake Mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Nam. 55

Banda la Skuli Jambangome

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Wananchi wa Jambangome katika Jimbo la Chambani wakiitikia wito wa Serikali walijenga banda la skuli lenye vyumba vine vya kusomea na ofisi mbili, ili kuongoa tabu kubwa wanayoipata watoto wao kufatia masomo katika Skuli ya Mizingani ambayo iko mbali mno. Katika mwezi wa Januari, 2011, Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alikuwa Mgeni Rasmi wa kuweka jiwe la msingi la jengo hilo na aliahidi kuchangia bati 300 na tayari ameshatekeleza ahadi hiyo muda mrefu sasa.

(a) Mhe. Waziri, kwanini hadi leo Serikali haijakamilisha ujenzi wa jengo hilo.

(b) Wizara haioni inavunja moyo juhudi za wananchi wa Jambangome ambao watoto wao wengi wanakosa masomo kutokana na ukosefu wa sehemu ya kusomea.

(c) Ni lini watu wa Jambangome watarajie kukamilishiwa banda hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye sehemu (a) na (b) na (c). Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba wananchi wa Jambangome katika Jimbo la Chambani wameitikia wito wa Serikali wa kuanzisha ujenzi wa madarasa manne mapya na ofisi mbili ili kuondoa tatizo la watoto wao kutembea masafa marefu kwenda kusoma katika Skuli ya Mizingani. Pia ni kweli Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alitoa ahadi wa kuchangia bati 300 katika sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi wa jengo hilo Januari, 2011. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza na

kumshukuru Mhe. Nassor Mazrui kwa kutimiza ahadi yake ya kutoa msaada huo wa mabati. Baada ya maelezo hayo sasa naomba nijibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Jengo hilo halijakamilika kutokana na wizara kutokuwa na fedha za kutosha katika kifungu cha ujenzi wa skuli za msingi ukilinganisha na wingi wa madarasa yanayohitaji kukamilishwa.

b) Wizara haiwavunji moyo wananchi wa Jambangome kwa kuchelewa kukamilisha jengo hilo kwani wananchi wanaelewa kwamba wizara inajitahidi kuyakamilisha majengo hayo katika sehemu mbali mbali za nchi yetu. Tunawaomba wananchi waendelee kuwa wastahamilivu.

c) Wizara imepata fedha katika kifungu hicho na hivyo kazi za uezekaji wa jengo hilo zitaanza katika mwezi wa Februari, 2012 mara tu baada ya taratibu za ununuzi wa vifaa na kumpata mwezekaji zitapokamilika. Ni matarajio yetu kuwa jengo hilo litakamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2012.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kuwa wizara sasa imepata fedha na amesema uwezekaji wa banda hilo unatarajiwa kuanza mwezi wa Februari na kumalizika mwezi wa Machi, 2012. Je, ni mwezi gani ndani ya mwaka huu wizara inalikabidhi banda hili kwa wananchi ili watoto wao waweze kusoma.

b) Kwa kuwa Mhe. Waziri wa Biashara Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alitoa huba ya bati 300 kwa wananchi wa Jambangombe. Je, wizara iko tayari thamani ya bati hizo kuzirejesha kwa wananchi wa Jambangome angalau kuanzisha msingi wa jengo jengine.

c) Kama wizara haikuwa tayari kufanya hivi kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimezungumza kwenye jibu mama kama skuli hiyo tunatarajia kuimaliza mwezi wa Machi, 2012. Kwa hivyo, mara tu baada ya kumaliza skuli hiyo tutaikabidhisha kwa wananchi, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mpaka mwezi wa Machi bado tutakuwa tunapokea wanafunzi wa darasa la kwanza kutokana na kuwa skuli zetu nyingi zina upungufu wa madarasa na tuko katika jitihada ya kuezeka madarasa hayo kwa hivyo mpaka mwezi wa Machi tutakuwa bado tunapokea wanafunzi ili waendelee na masomo yao ya darasa la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala jengine kama wizara itakuwa tayari kurudisha pesa za hubwa ambazo amezitoa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuwapa wananchi na wanafunzi wa Jambangome. Mhe. Mwenyekiti, wizara haitotoa pesa hizo zilizotolewa kwa sababu sera ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya 2006 ni wananchi kujenga na wizara kumaliza ujenzi huo.

Mhe. Mazrui ni mwananchi, ni mzazi na ni kiongozi kwa hivyo alichofanya ni wajibu wake kwa nchi yake. Mhe. Rais amekuwa akituhimiza sana juu ya yale ambayo tunayaweza kuyachangia wenyewe tusisubiri misaada kutoka nje. Kwa hivyo, Mhe. Mazrui ametimiza wajibu wake na naomba waheshimiwa wengine waige mfano huo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba hatutorudisha kwa sababu nataka niwarudishe Wajumbe wa Baraza hili tukufu katika bajeti yetu ya mwaka huu kwenye ukurasa wa 18-19 pale tulizungumza kuhusu kazi ambazo zinatukabili katika mradi wa elimu ya msingi, tulisema kama mwaka huu tunahitaji kuezeka madara 200, lakini pia tulisema pia tuna nyumba za walimu 3, tuna ununuzi wa vikalio na ni bilioni 1 tu ambayo tumeomba katika kazi zote hizi.

Mhe. Mwenyekiti, haidhuru kutakuwa na fedha za wahisani lakini mchango wetu kama wizara ni bilioni 1 tu. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi aone uzito ambao tunao katika wizara yetu na akubaliane na sisi kuwa fedha hizo ziendelee katika kuezeka madarasa mengine ambayo wanafunzi wetu wanahitaji sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno na kwa kuwa umeahidi itakapofika Machi 2012 banda hili litamalizika.

Je, ahadi hii haitokuwa kama alivyoahidi aliyekuwa Mhe. Waziri wa Elimu Mhe. Haroun Ali Suleiman alipoahidi kuwa kuezeka jengo lililopo Skuli ya Ngambwa tangu 2009 hadi leo hii halijaezeka. Je, kwa kufanya hivyo haitovunja moyo wananchi na watoto wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kama wizara ambavyo imeahidi basi itakapofika mwezi wa Machi tutatekeleza na tutakabidhi wazazi ili wanafunzi wetu waanze kusoma.

Nam. 106

Chuo ca Kiislam Micheweni Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua hatua mbali mbali ikiwemo kuimarisha vyuo ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira mazuri Unguja na Pemba.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuondoa matatizo ya wanafunzi wa Chuo cha Kiislamu Micheweni ambao wanasoma katika mazingira magumu na usalama wa mali zao na wao wenyewe unaanza kupungua kutokana na matatizo yanayokikabili chuo hicho.

(b) Kwa kuwa Serikali inatenga fedha kila mwaka na shilingi milioni 50 zilitengwa kwa ajili ya chuo hicho. Je, Serikali imewapatia kiasi gani kati ya hizo fedha zilizotengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza napenda kutoa maelezo ya yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imechukua hatua mbali mbali katika kuimarisha mazingira ya vyuo ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira mazuri. Baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Serikali inayo jitihada ya kuondoa matatizo katika vyuo vyote kikiwemo Chuo cha Kiislamu Micheweni. Kwa mfano, katika chuo hicho mwaka wa fedha 2009/2010, jumla ya Tsh. 25 milioni zilitumika kwa ajili ya kufanya ukarabati wa madarasa, dakhalia, ikiwemo utengenezaji wa vyoo, ujenzi wa ukumbi na ujenzi wa mageti katika dakhalia na dari ya jengo la utawala. Pia, kazi za upigaji wa matofali kwa ajili ya

ujenzi wa ukuta wa kuzunguka chuo zimeanza kwa upigaji wa matofali 100 ya kuanzia. Aidha, chuo kimepatiwa gari nyengine ndogo aina ya SUZUKI ili kusaidia mahitaji ya usafiri badala ya kutumia gari aina ya Tata wakati wote. Kwa kiasi kikubwa mazingira ya Chuo cha Kiislamu Micheweni yameweza kubadilika na kuwa mazuri zaidi.

Kwa mwaka 2011/2012, mradi wa ujenzi wa Chuo cha Kiislamu Micheweni umetengewa jumla ya shilingi 50 milioni kwa ajili ya ujenzi wa uzio na kuendelea na ukarabati wa jengo. Jumla ya shilingi 15 milioni zimepelekwa Pemba kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika chuo hicho na wizara itaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kuimarisha zaidi mazingira ya vyuo vyetu Unguja na Pemba. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ilipotembelea chuo kile kwa kweli hali ya siku ile ilikuwa hairidhishi ikiwemo kutokuwa na milango na makomeo.

Je, serikali itachukua hatua gani ya dharura ya kukabiliana na tatizo hilo hasa ukizingatia skuli hiyo ina wanafunzi wa kike na inahitaji usalama wa hali ya juu.

Pili, kwa kuwa bajeti wanazitengeneza wenyewe na wametenga shilingi 50 milioni kuna sababu gani ya kuwapa shilingi 15 milioni wale mpaka muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikiri kwamba ni kweli Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ilikwenda kutembelea katika chuo hicho katika kutekeleza kazi zake za ufuatiliaji wa ahadi za serikali. Kama ambavyo nimezungumza katika suala

langu mama kama ni kweli pia wizara ilitenga shilingi 50 milioni kwa ajili ya ukarabati wa chuo hicho pamoja na ujenzi wa ukuta.

Nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba pesa hizo ambazo tumezipeleka zitafanya yale mambo ya lazima ambayo yanahitajika kwa kipindi hiki yafanywe ikiwemo kujenga ukuta. Tunajua shilingi 15 milioni haziwezi kujenga ukuta lakini tutaendelea na ufyatuaji wa matofali, lakini pia katika zile sehemu ambazo zinahitaji vikomeo basi zitatumika pesa hizo.

Hata sisi Mhe. Mwenyekiti, tunatamani tuweze kuzipata shilingi 50 milioni kwa pamoja ili kukamilisha ule mradi ambao tumekusudia katika chuo kile. Lakini hizi fedha zinatokana na tunavyoingiziwa na mapato ya serikali yanavyoingia mwezi hadi mwezi. Niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi kama tutahakikisha kuwa mazingira ya chuo kile yanaimarika siku hadi siku.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri anasema kuwa wamejitahidi, lakini inaonekana kwamba pamoja na mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, pamoja na sehemu zilizofanyiwa ukarabati kwa mfano kwenye mapaa na ukuta ulioko juu ya mapaa yale hadi leo hii mabanda yale yanaendelea kuvuja na wanafunzi wanazalilika sana.

Je, atakubaliana nami kwamba wizara yake haina usimamizi mzuri inapofanya kazi za wizara. Hilo moja.

Pili, Chuo cha Micheweni Mhe. Mwenyekiti, kiko mbali na hakina majengo ya walimu, kwa hivyo, walimu hulazimika kufanya kambi kwa ajili ya kutoa taaluma kwa wanafunzi wetu na wizara yake iliahidi kutoa *disturbance allowance* kwa wale walimu wanaotoka Mkoani, Chake Chake na kupiga kambi katika chuo kile kwa ajili ya kufundisha, lakini huu ni karibu mwaka wa

pili hawajalipwa *disturbance allowance* yao. Je, kwa kufanya hivyo si kuwadhulumu walimu wetu.

La mwisho ni kwamba haki ikichelewa kutolewa ni kwamba haikutolewa kabisa. Je, kuendelea kuwanyima walimu hawa haki zao si kwenda kinyume na haki za binadamu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilifanya ziara na nilitembelea Skuli ya Micheweni na niliiona hali halisi ilivyo. Kwanza niwapongeze sana Maafisa wangu wa Wizara ya Elimu Pemba namna walivyofanya kazi ya ukarabati katika maeneo mbali mbali kwenye majengo yale.

Ni kweli lipo tatizo la mabati kuvuja, mbali ya sehemu zilizofanyiwa ukarabati lakini bado liko tatizo la mabati kuvuja. Hilo nakubaliana naye na wizara yangu itajitahidi kuona kwamba tunabadilisha kidogo kidogo mabati katika skuli ile ili tuondoe hii shida ya kuvuja.

Pili Mhe. Mwenyekiti, mimi nawapongeza sana walimu kwa kuanza kusomesha pale kwa kupiga kambi. Inaonesha hawa walimu wamekubali ule utaratibu wa kuwasomesha watoto kwa moyo wa dhati kabisa kwa hivyo, nawapongeza sana. Ila suala kwamba hawajalipwa fedha zao Mhe. Mwenyekiti, mimi nitafuatilia na kama kweli hawajafanyiwa hivyo basi wizara yangu itachukua hatua ya kuwalipa.

Nam. 6

Utekelezaji wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu katika Wizara za Serikali

Mhe. Raya Suleiman Hamad – Aliuliza :-

Mhe. Waziri, wizara zote za serikali chini ya masharti ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu zitaanzisha na kuweka mtu maalum (Afisa Mratibu) kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji na ufuatiliaji wa masharti ya Sheria hiyo, Je, Wizara ngapi zimeshatekeleza agizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu :-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kujibu swali Nam. 6 la Mhe. Raya Suleiman Hamad kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mjumbe aliyeuliza swali hili, kwamba kwa mujibu wa Sheria No.9 ya mwaka 2006 ya Haki na Fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu, Ibara namba 21 ndio inayoagiza Wizara za Serikali Zanzibar kuweza kuanzisha na kuweka mtumishi maalum (Afisa Mratibu) kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji na ufuatiliaji wa masharti ya sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa rasmi kwamba wizara na ofisi zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tayari zimeshaanzisha na kuweka Maafisa Waratibu hao. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatoa shukrani zake za dhati kwa mashirikiano tuliyoyapata kutoka wizara na ofisi hizo za serikali, lakini pia, napenda kutoa wito kwa Makatibu Wakuu wa wizara na ofisi zote zinazopanga mipango na Bajeti ya Wizara zao wahakikishe suala la Watu wenye Ulemavu linajumuishwa kutokana na mahitaji ya Watu wenye Ulemavu katika wizara hizo. Pamoja na hayo, naomba tuzidishe mashirikiano kwa lengo la kukuza na kuinua haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu hapa nchini.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweza kutupatia afisa

huyu, lakini bado ikiwa mawizarani tayari afisa huyu keshakuwepo lakini watu wenge wenye ulemavu bado hawajajua na ikiwa wapo vile vile hawajatekeleza kazi zao ipasavyo. Tunaomba Mhe. Waziri uwe kigezo na kuweza kutupatia maafisa hawa na waweze kutufikia sehemu mbali mbali kwa kuweza kutufahamisha yale majukumu yetu tuliyojipangia juu yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wake nauchukua na ofisi yangu tayari imekaa na wataribu hawa wa ofisi mbali mbali lakini tutaendelea kukaa nao na kuwafahamisha jinsi gani bora ya kutimiza majukumu yao.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa madhumuni makubwa ya waratibu hawa ni kutekeleza hiyo sheria, na wizara hii ndio inayohusika. Je, Mhe. Waziri amejipanga vipi ili kuandaa mkusanyiko utakaowakusanya waratibu hawa pamoja na wale viongozi wenye ulemavu ili kuelekezana na kujua ni mtazamo gani wa pamoja wanaotaka kuufuata.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuarifu Mheshimiwa kwamba tayari ofisi kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu imeshakaa na waratibu hawa na kueleza jinsi gani wanaweza kutekeleza kazi zao vilivyo. Pia utaratibu unaandaliwa wa hivi karibuni Baraza la Watu wenye Ulemavu ambao ndio hasa wanaosimamia majukumu ya kuona kwamba sheria nayo inatekelezwa ipasavyo watakaa na waratibu hawa katika kuhakikisha lengo linafanikiwa.

Nam. 4

Ukosefu wa Mazingira Rafiki kwa Watu wenye Ulemavu

Mhe. Raya Suleiman Hamad – Aliuliza:-

Mhe. Waziri watu wenye ulemavu wa viungo (wanaotumia vigari na magongo) wanaendelea kupambana na vizuizi vinavyotokana na ukosefu wa mazingira rafiki yanayowawezesha kuingia katika majengo ya Umma kwa ajili ya kupata huduma. Je, wizara yako kama wizara mama inachukua hatua gani kuondowa vikwazo hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali Nam. 4 la Mheshimiwa naomba kwanza ninukuu sheria Nam, 9 ya mwaka 2009 ya Haki na Fursa Sawa kwa Watu wenye Ulemavu ambayo imepitishwa na Baraza lako tukufu kama hivi ifuatavyo:-

Ibara ya 12 mbayo inahusiana na upatikanaji na uwezo wa kufikia huduma, kifungu 12(1) kinasema,

> "Watu wenye Ulemavu watakuwa na haki ya kutopata kuzuizi kuwa na mazingira rafiki yatakayowezesha kuwa na fursa ya kufika katika nyumba za umma na vifaa kwa ajili ya matumizi ya umma".

Kifungu cha 12(2) kinasema:

> "Masharti ya kifungu cha kwanza cha kifungu hiki yatatumika na kuwabana wamiliki wa majengo ya umma yaliyopo na huduma kwa matumizi ya umma".

Kifungu cha 12(3) kinaeleza,

> "Wasanifu majengo, wahandisi wa ujenzi na watu wengine wanaohusika na usanifu na ujenzi wa majengo watalazimika kuzingatia upatikanaji wa vifaa wakati wanaanza taratibu za kuandaa michoro na kuhakikisha kwamba majengo yote

mapya yanakwenda sambamba na michoro yenye lengo la kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu".

Mhe. Mwenyekiti, baada ya nukuu hiyo naomba sasa kujibu swali Nam. 4 la Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ibaya hiyo pamoja na vifungu vyake vinatoa fursa kwa watu wenye ulemavu wakiwemo wenye ulemavu wa viungo wa kuweza kufikia na kutumia majengo yanayotoa huduma kwa umma. Kwa mujibu wa sheria hiyo ya Watu wenye Ulemavu, watu wenye ulemavu hapa imekusudiwa wenye ulemavu wa aina zoe ambao ufikiaji na utumiaji wa majengo hayo utakuwa umetoa haki kama wasanifu majengo na wahandisi wa ujenzi na watu wengine watazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu wa viungo.

Mhe. Mwenyekiti, vifungu vya sheria vinatoa ulazima kwa wahusika kuweka mazingira mazuri kwa watu wenye ulemavu ikiwemo ulemavu wa viungo kama vile kuwekewa utelezi, vikamatio, vyoo maalum kwa ajili ya matumizi yao, kuwekewa *lift* na kuwa na koridoo pana kwenye majengo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nitoe nukuu ya Ibara ya 13 kama hivi ifuatavyo:-

Ibara ya 13 inahusiana na upatikanaji wa viwango. Ibara ya 13(2) kinasema kwamba, "Sharti la upatikanaji wa viwango hivyo litajumuisha pia katika michoro na ujenzi wa mazingira yenyewe".
Mhe. Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na ofisi yangu pamoja na Baraza la Watu wenye Ulemavu ni kutembelea majengo yanayojengwa na kuweza kubadilishana mawazo pamoja na kutoa ushauri wa kuzingatia hali hiyo. Kwa mfano, Baraza la Watu wenye Ulemavu lilitembelea Bodi ya Mapato Zanzibar kwa kushauriana nao na kusisitiza kuhusu suala zima la jengo lao jipya

kuweza kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu na mfano huu kwa sasa tunaweza kuona kwamba jengo hili lililofunguliwa limeweza kukidhi na kuingiza mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, pia watendaji wa idara wameonana na Mkurugenzi Idara ya Ujenzi kwa lengo la kushirikiana na Msanifu Mkuu wa idara hiyo ili kuweza kuandaa mkakati utakaoweza kusaidia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Mhe Mwenyekiti, vile vile ofisi yangu imetoa agizo kwa Makatibu Wakuu wa Wizara na Afisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwaomba wanaojenga majengo mapya au kufanyia marekebisho majengo yao, wazingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Kwa upande mwengine ofisi yangu kupitia Baraza la watu wenye ulemavu litaendelea kuchukua hatua mbali mbali itakazoona zinafaa katika kuhakikisha watu wenye ulemavu wanayafikia majengo yanayotoa huduma ikiwemo pamoja na kuzungumza na viongozi wa taasisi husika ambazo zinashughulikia upitishaji wa michoro, kutopitisha michoro yote ambayo haitoi mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kuingiza kipengele maalum katika sheria au sera juu ya kutopitisha michoro ya majenzi ambayo haizingatii mahitaji ya watu wenye ulemavu ni muhimu sana. Pamoja na hayo, suala hili litawezekana pindipo sheria au sera inayohusu majengo itaingiza moja kwa moja kipengele cha kutopitisha michoro hiyo.
Hivyo ofisi yangu itashauriana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuangalia tena sera au sheria inayohusu majenzi ambayo moja kwa moja itaweza kuingiza kipengele hicho muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kutoa wito kwa ofisi na wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zile za binafsi zinazotoa huduma kwa jamii kuweza kuweka mazingira rafiki ili ndugu zetu wenye ulemavu waweze kuyafikia majengo hayo kwa usalama zaidi.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, pamojana maneno mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri kidogo nasikitika. Tangu mwaka 2005 nilipoingia tunapigia kelele majengo na ikiwa ni jingo moja jipya ni jengo la Baraza la Wawakilishi, bado lina kikwazo sana kwa watu wenye ulemavu.

Leo Afisa Mdhamini wangu wa Walemavu kaja hapa mimi mwenyewe naona imani kwa sababu mimi najiona mzima kuliko yeye nataka nimbebe nimpeleke huko juu. Hii ni hali halisi, siku nyengine atakuja mtu mwengine ambaye anakwenda kwa mikono na miguu hili jingo halina kipandio wala hata kibandiko cha kusema hii *lift* ya kumpeleka mtu huko juu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri katika suala hili alichukuwe kwa makini. Kwa sababu mimi ni Mwakilishi wako nakwenda kwenye kamati mbali mbali sehemu ya Unguja, Mheshimiwa majumba hayana *lift* na mengine mapya yamejengwa hata ile *lift* ya kubandika nje hakuna tunapanda kwa ngazi siku nyengine nabakia kwenye gari taarifa nikaletewa tu mimi huwa sipandi. Kwa hivyo, tunaiomba serikali iweze kutoa huduma za watu hawa na hata vyoo katika maofisi, sisi tunakwenda kwa vigari mtu atakwendaje kwa kigari choo kimebanwa ataingia vipi na kigari chake. Tunaomba majengo yabadilishwe mara moja tuweze kufikia na sisi katika huduma za watu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpa pole sana kwa usumbusu wanaoupata na atakumbuka vyema mimi nilikuwa ni mmoja wapo ambaye tulikuwa tunapiga kelele kwa pamoja juu ya ujenzi wa jengo hili la Baraza la Wawakilishi ambalo nalo

halikuzingatia masharti. Naomba sana viongozi wa muhimili huu walione hilo na waweze kufanya marekebisho ili wenzetu wasipate tabu katika kufanya shughuli zao.

Kwa upande wa ofisi yangu Mhe. Raya nimezungumza katika *paragraph* ya mwisho kabisa kwamba hivi sasa tunaangalia uwezekano wa kuweza kuzuiya kupitisha mchoro wowote ambao unahusiana na kutoa huduma kwa jamii ambao hautazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Kwa hivyo, sheria hiyo tukiipata itatusaidia sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa Mhe. Waziri wizara yake ndiyo inayosimamia sheria hii Nam. 9 ya mwaka 2006 pamoja na utekelezaji wake, na kwa kuwa ni kosa la jinai kwa taasisi yoyote kujenga jengo la umma bila ya kuzingatia watu wenye ulemavu, na kwa kuwa bado kuna taasisi zinajenga majengo ya aina hiyo bila ya kuzingatia sheria hii Nam.9 ya mwaka 2006, na kwa kuwa kuna majengo mengi yameshajengwa tokea ilipopitishwa sheria hii hadi leo wanaendelea kujenga.

Je, Mhe. Waziri ni taasisi ngapi zimeshafikishwa Mahkamani kutokana na kosa kama hilo na ni hukumu gani ambayo imetolewa. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii ya upatikanaji wa fursa na haki sawa kwa watu wenye ulemavu haikueleza adhabu ambazo wale ambao hawakuzingatia taratibu hizi za majenzi kama itakuwa ni kesi ya kuweza wao kushtakiwa na kupewa adhabu. Lakini ninachomuomba Mhe. Mwakilishi asubiri aone pale ambapo tutaweza katika hatua ya kwanza kabisa kushauriana na

Wizara ya Ardhi kuizuia kabisa michoro ili matatizo hayo yasitokee.

TAARIFA

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kitu Afisa Mdhamini ni Mkurugenzi wangu aliyeko juu.

Nam. 68

Suala la Ajira kwa Wanawake

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Utafiti unaonyesha kuwa katika maeneo ya Mjini idadi ya wanawake wasio na ajira ni kubwa kuliko wanaume.

Je, serikali ina mkakati gani wa kuwanyanyua wanawake katika ajira ili waweze kuboresha maisha yao ikizingatiwa kuwa wanawake ndio wanatunza familia.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, suala la ukosefu wa ajira ni tatizo la kijamii ambalo limeikumba Zanzíbar na sehemu zote za dunia, yakiwemo mataifa yaliyoendelea kama vile Marekani, Ufaransa na mengineyo. Hali hii imesababishwa na mambo mengi ikiwemo uchache wa viwanda, kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi, kiwango kidogo cha ujuzi katika baadhi ya fani muhimu na ukuaji wa haraka wa teknolojia kwa kuyataja machache. Taarifa mbali mbali zilizopo kuhusu ajira zikiwemo zile zinazotolewa na Shirika la

Kazi Duniani zinaonesha tatizo hili kuyakumba makundi mawili makuu Ambato ni ya wanawake na vijana.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba taarifa za utafiti hapa Zanzíbar zinaonesha kuwa katika maeneo ya Mjini idadi ya wanawake wasio na ajira ni kubwa kuliko ya wanaume. Kwa kutambua tatizo hili,

Sera ya Ajira Zanzíbar imetoa kipaumbele kwenye suala zima la kuwezesha wanawake kupata ajira. Aidha, mikakati maalum imewekwa ndani ya sera hiyo kuwezesha hilo ikiwemo kushajihisha upatikanaji wa fursa zaidi za elimu kwa wanawake ili waweze kumudu ushindani kwenye soko la ajira pamoja na kuwajengea uwezo wa ujasiriamali ili waweze kujiajiri na kujipatia kipato.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali za Mikoa na Wilaya imo katika zoezi la kukusanya taarifa kuhusiana na hali za wananchi kiajira, hasa wanawake na vijana. Taarifa hizo zimeanza kukusanywa katika Mkoa wa Mjini Magharibi na zinaendelea katika Mikoa iliyobaki. Upatikanaji wa taarifa hizo utaisaidia wizara kuweza kupanga mikakati madhubuti ya kuwawezesha wananchi kujiajiri au kuajiriwa kadri fursa zitavyopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, pia wizara kwa kushirikiana na Serikali za Moka wa Mjini Magharibi Unguja na Mkoa wa Kusini Pemba imeanzisha Kamati za Uzalisaji wa Ajira na Uwezeshaji. Lengo la kuundwa kwa kamati hizo ni kubainisha na kufuatilia fursa za ajira na uwezeshaji katika maeneo yao ili iwezeshe kubuni mikakati ya uzalishaji ajira zaidi kwenye maeneo hayo. Kamati hizi pia zitaundwa kwenye Mikoa iliyobaki ya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendelea kutoa taaluma kwa vikundi mbali mbali vya ujasiriamali ambavyo vingi ni vya wanawake, ili

kuviimarisha viweze kuzalisha zaidi na kuwaongezea kipato kitachosaidia kunyanyua maisha yao na pia kutunza familia zao. Sambamba na hayo, wanawake pia wamekuwa wakifaidika na mikopo inayotolewa kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri na kuimarisha shughuli zao za kiuchumi. Hadi kufikia mwezi wa Novemba 2011, jumla ya wanawake 4,732 wamefaidika na mikopo kupitia Mfuko wa AK/JK na ule wa kujitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za serikali katika utekelezaji wa programu za kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuwaongezea fursa za ajira. Tunategemea hatua tunazozichukua zitasaidia kufanikisha malengo ya kunyanyua ubora wa maisha ya wanawake na wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu marefu ya Mhe. Waziri nia maswali mawili ya nyongeza. Mfuko wa kuwasaidia wajasiriamali ulianzishwa na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume, lengo lilikuwa ni kusaidia wajasiria mali. Je, ni kiasi gani kimeshatumika hadi sasa na kiasi gani kimerudishwa hadi hivi sasa.

Pili, tangu kuanza kutolewa fedha hizo ni bidhaa gani ambazo zimekuwa zikizalishwa na vikundi hivyo na serikali imepata kiasi gani cha kodi na wahusika na thamani ya bidhaa hizo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema kwamba Mfuko huu ulianzishwa na marais kama Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume. Jumla ya pesa ambazo walizitoa kila mmoja wao ni shilingi 600 milioni na pesa hizo zikapelekwa Benki ya PBZ kwa lengo la kuwa pesa zile ziwe ni

guarantee na benki ikatuhakikishia kwamba wao watatoa bilioni mbili na 400 milioni nalo zoezi hilo likafanyika.

Hadi wakati huu ninapozungumza jumla ya shilingi bilioni moja na 400 milioni zimetolewa, zilizobakia ni shilingi bilioni mbili na 200 milioni ambazo hizo sasa hivi tayari kuna maombi kama mia mbili ambayo yako PBZ. Lakini juzi nilizungumza hapa nikasema kutokana na urasimu unaotokea benki na ufuatiliaji kiasi ambacho ulipaji unakuwa ni hafifu. Kuna mazungumzo yanakwenda na pengine tutayakamilisha hivi karibuni kuhakikisha kwamba pesa zile sasa zinasimamiwa na wizara yangu moja kwa moja badala ya kusimamiwa na *PBZ* kama ilivyo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, pesa zile zimesaidia wajasiriamali katika kuzalisha bidhaa mbali mbali kama vile sabuni, mafuta, vyakula ambazo zimewasaidia sana wajasiriamali wetu. Siwezi kujua zimepatikana kiasi gani kwa sababu faida hiyo wanahesabu wao wenyewe wajasiriamali, isipokuwa tunachokihitajia sisi upande wetu ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwasaidia na lengo la serikali kupitia Wizara hii tutaendelea kuwasaidia wananchi wote wanawake, wanaume, vijana, watoto na wengineo.

Nam. 117
Mtaro wa Migombani

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:

Kijiografia Jimbo la Mpendae limezungukwa na mabonde ambayo wakati wa mvua husababisha wakaazi wake kuishi bila ya amani katika Shehia ya Migombani kutokana na ukosefu wa msingi wenye uwezo mkubwa wa kupitisha maji hayo haraka.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuufanyia matengenezo na kuupanua msingi wa maji Migombani.

(b) Je, kwa sasa msingi huo una wafanyakazi wangapi wa kudumu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 117 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Jimbo la Mpendae limezungukwa na mabonde ambayo wakati wa mvua wananchi wa maeneo ya karibu na mabonde hayo huathirika na maji ya mvua yanayotuama na hasa katika Shehia ya Migombani.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali imelizingatia kwa makini tatizo la kuwepo kwa uwezo mdogo wa msingi wa maji ya mvua wa eneo la Migombani. Kwa kuelewa hilo, Serikali imepanga kuujenga upya msingi mkubwa wa maji ya mvua kutoka Magomeni kupitia kwa Biti Hamrani, Jang'ombe, Migombani Jeshini hadi Kilimani. Msingi huo utakuwa na urefu wa mita 4,628 na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka huu kupitia mradi mkubwa wa kuimarisha huduma za Mjini unaoitwa *Zanzibar Urban Service Project (ZUSP).*

Mhe. Mwenyekiti, mradi tayari umeshaanza na hatua za awali muhimu za mwanzo katika utekelezaji ni ununuzi wa zana nzito na nyepesi zitakazotumika katika uchimbaji wa ujenzi wa msingi huo. Mchakato wake tayari umeshaanza wa kuwapata hao wakandarasi na wanunuzi.

(b) Utaratibu unaotumika wa kusafisha misingi ya maji ya mvua Mjini ukiwemo usafishaji wa msingi wa Migombani ni kwa kutumia kikundi kimoja cha wafanyakazi wapatao saba ambao husafisha kwa kupitia misingi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupitia Mhe. Mwakilishi watusaidie wale wananchi wanaoishi karibu na eneo hili waache kutupa taka ndani ya msingi huu bali watumie majaa yaliyopo katika kutupa taka zao.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa hakuna kikosi chochote katika hao watu saba aliosema kilichopita katika msingi huo na kufanya usafi kwa muda mrefu kwa hivi sasa.

Lakini (b) Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa hata Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alipotembelea pale akatoa ahadi ya kuweza kutengeneza ile sehemu ndogo ambayo iliharibika mpaka sasa wizara yako imekaa kimya. Kuendelea kukaa kimya si kuwadharau wananchi wa Jimbo la Mpendae na kudharau kauli halali iliyotolewa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nakiri kwamba hali ya msingi huu si nzuri na si ya kuridhisha mimi mwenyewe nimeupitia na nimeona hali ilivyo. Lile ombi nililotoa mwanzo Mhe. Mwenyekiti, kumuomba Mhe. Mwakilishi tusaidiane kwa sababu hili suala ni letu, ni la jamii, tusaidiane kwanza watu wasitupe taka ndani ya msingi.

Tatizo kubwa tulililoligundua kwamba watu wanatumia msingi kama ndio jaa, utakuta msingi mna taka, mna vipolo, chupa na kila aina ya uchafu. Sasa naomba sana kupitia kwako Mhe. Mwakilishi wa eneo hili sisi tuko tayari kufanya kazi na wewe tusaidiane kuwaelimisha jamii watupe taka kwenye majaa yaliyowekwa. Kama nilivyosema tutajitahidi tushirikiane sote kwa pamoja kuweka usafi na sisi tutatimiza wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, la pili kuhusu ahadi aliyoitoa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nakiri kuwepo ahadi hiyo mimi nilikuwa sijaipata lakini leo umenijulisha naomba tukitoka hapa mimi na wewe tukae chini tupange mikakati jinsi ya kuitekeleza.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza baada ya majibu mazuri ambayo ameyatoa Mhe. Waziri sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya wananchi kukaa kwa muda mrefu pamoja na kusubiri ili kuweza kuondoshewa tatizo hilo ambalo linawakabili, wananchi hao ambao wako mpakani baina ya Jimbo la Mpendae na Kikwajuni sasa wameamua kutumia nguvu zao kwa ajili ya kutengeneza eneo hilo angalau waweze kupata eneo la kuvuka kutoka eneo moja kwenda eneo jengine.

Sasa je, Mhe. Waziri, Wizara yako itakuwa tayari kuwasaidia wananchi ambao tayari wanaanza leo kutoa nguvu zao na kutengeneza eneo angalau la kupitia na nyinyi baadae mkaendelea nalo zaidi ili kuwaunga mkono wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa kushajihisha juhudi hizi za wananchi za kuanza kujisaidia wenyewe na hiyo ndio *spirit* tunayoitaka. Serikali ina mengi ya kufanya lakini tukiona kidogo wanakuja basi tuwahi sisi na serikali itakuja kumalizia.

Sasa naomba nimpongeze sana kwa juhudi hiyo na nakuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba mimi niko tayari tukitoka hapa twende tukapange mikakati ya kumalizia hiyo juhudi iliyoanzwa.

Nam. 124

Jengo la Afya ya Akili Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kuna taarifa kwamba Jengo la Afya ya Akili Pemba linalojengwa kwenye eneo la Hospitali ya Wete Pemba linajengwa kwa gharama ya US$ 450,000 sawa na Tshs. 765,000,000/=.

(a) Mhe. Waziri, uamuzi wa kujenga jengo hilo dogo la chini kwa gharama kubwa kiasi hicho ulifikiwaje.

(b) Inasemekana kwamba uongozi wa Wizara ya Afya Pemba haukushirikishwa katika hatua za tathmini ya tenda ya ujenzi huo kwa nini.

(c) Je, Wizara yako itakuwa tayari kulifanyia ukaguzi wa thamani *(value for money auditing)* jengo hilo ili kuondoa shaka iliyopo ya ubadhirifu wa fedha za umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 124 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ningependa kutoa taarifa ndogo tu kwamba Jengo la Afya ya Akili linalojengwa kwenye eneo la Hospitali ya Wete Pemba limejengwa kwa gharama ya US$ 450,000 sawa sawa na Tshs. 765,000,000/= si sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo napenda nijibu maswali ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

(a) Uamuzi wa kujenga Jengo la Afya ya Akili Pemba linalojengwa katika eneo la Hospitali ya Wete ni sehemu ya mpango wa Wizara kusogeza huduma kwa karibu kwa wagonjwa wa akili kutoka Pemba ili

kuondoa usumbufu kusafirishwa hadi Unguja. Taratibu za kufikia uamuzi huo zilifuatwa kwa hatua tatu muhimu nazo ni kutangaza zabuni, kufungua zabuni na kuwatathmini waombaji na kuamua nani apewe zabuni hiyo.

(i) Zabuni ilitangazwa kwenye gazeti la *Guardian* tarehe 12 Novemba, 2010.

(ii) Wakandarasi 6 walijitokeza kwenye zabuni hiyo nao ni *Rans Company* ya Zanzibar, Building Hardware ya Morogoro, *Stanc Technic* ya Arusha, *Siha Enterprise* ya Dar es Salaam, *Assert Builders* ya Dar es Salaam, *AIS Limited* ya Dar es Salaam. Walionunua na kurejesha zabuni ni 5, *AIS* hakurudisha. Zabuni ya juu ilikuwa milioni 554,908,629/= na ya chini ilikuwa milioni 439,266,080/= shilingi za Kitanzania pamoja na *VAT*.

(iii) Kikao cha tarehe 13 Disemba, 2010 kilipitisha zabuni. Zabuni ilithibitishwa tarehe 6 Januari, 2011.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kilichosemekana ni sahihi kwamba uongozi wa Wizara ya Afya Pemba haukushirikishwa kwa sababu zabuni zinapitishwa na Bodi ya Wizara ambayo Mwenyekiti wake ni Mkurugenzi Mkuu, Wajumbe wake ni Wakurugenzi wa Wizara ya Afya, sekretarieti yake ni Kitengo cha Manunuzi cha Wizara *(Procurement Unit)*, *Engineer* wa *ADB* kwa sababu yeye ndio aliyetoa fedha ndie aliyehusika kuchagua mkandarasi na Mratibu wa Afya ya Akili ambaye ndie mhusika mkuu. Hao niliowataja ndio waliotakiwa kuwepo katika kikao cha maamuzi kwa mujibu wa sheria ya manunuzi katika Wizara ya Afya kwa sababu

Hospitali ya Wete si hospitali ya Pemba bali ni hospitali ya Wizara ya Afya.

(c) Wizara ya Afya inafanya kazi nilizozitaja kwenye maelezo yangu ya utangulizi na suala la kufanya ukaguzi ni la wakaguzi wa ndani na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sidhani kama ni sahihi kutumia fedha ikisha ukajikagua mwenyewe matumizi yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali alisema sidhani kama ni sahihi kutumia fedha ikisha ukajikagua mwenyewe matumizi yako.

(a) Je, Mhe. Waziri atakuwa yuko tayari kutoa mashirikiano na Kamati ya *PAC* kuchunguza mradi huo wa ujenzi ili kujua sababu zilizopelekea jengo hilo kuwa halilingani na thamani ya fedha licha kuwa ni mkopo wa fedha hizo.

(b) Kwa kuwa Wizara ya Afya ndio mhusika mkuu ilikuwaje ikakubali kupitisha zabuni ya kujenga jengo lenye uwezo wa kuhifadhi wagonjwa 16 tu wakati nilipokuwepo Chake Chake na Wete pekee ina wagonjwa wanaotembea mitaani zaidi ya 25.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kumsaidia Mhe. Naibu Waziri kwenye suala hili. Tunasisitiza kwamba si kawaida mtu kujikagua mwenyewe hasa kwa taratibu za serikali. Ni haki ya Mwakilishi kutaka masuala yachunguzwe lakini la kwanza anayestahiki ni *Controller Audit Department* ambao wakienda huko wakiona kuna haja ya kufanyiwa uchunguzi ndipo labda Kamati ya *PAC* au Baraza hili au Serikali inaweza kuunda tume. Hatuwezi tu kujichukulia amri

wenyewe kwa sababu tu tunaona mambo hayendi lazima tufuate sheria.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kama jibu alilotoa Mhe. Naibu Waziri ni kweli kwamba hospitali ya wagonjwa wa akili inayojengwa Wete ni hospitali ya Wizara ya Afya na si hospitali ya Pemba.

Lakini Pemba kuna waajiriwa wa Wizara ya Afya kama vile Afisa Mdhamini na baadhi ya wakurugenzi wapo pale.

(a) Je, kitendo cha kwamba mambo yote ya ujenzi wa hospitali ile kufanywa Unguja na wale kuwa ni wapokeaji tu wa vifaa si kuwadhalilisha watumishi wa Wizara ya Afya.

(b) Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mhe. Naibu Waziri kajibu kuwa kuna tenda ilitangazwa. Je, atakubaliana nami kwamba Wizara ya Afya hawakuwa makini walipotangaza tenda ile kwa sababu pale pale katika hospitali ya Chake Chake imejengwa maabara ya kisasa kabisa katika njia za msaada ambayo tayari ni ya kukabidhi tu, ni *well varnished* kwa thamani isiyozidi shilingi za Kitanzania milioni 150. Je, kutumia milioni 700 kwa jengo moja tena la chini si uharibifu wa fedha za walipa kodi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, tulisema hapa kwamba kutoa tenda ni taratibu za kisheria si suala la kumdharau mtu wala kumpendelea mtu. Sheria inasema kwamba Kamati ya Tenda ya Wizara Wakurugenzi ndio Wajumbe imetajwa kwenye sheria, haikusema kwamba Juma Duni Haji au Saleh Nassor Juma, kwa hivyo hakuna aliyedharauliwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kwamba kuna kituo chengine kimejengwa kwa thamani ya chini bado tunasema kama kuna wasi wasi huo taratibu za kisheria zifuatwe, *Controller* wa *Audit* aende huko akaone thamani yake na kama kuna haja basi iundwe kamati.

Nam. 63

Kuchelewa kuanza masomo

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma – Aliuliza:

Ni sababu zipi zilizopelekea kuchelewa kutoanza masomo kwa wanafunzi ambao wameshadahiliwa katika Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Waziri wa Kilimo na Maliasili) – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kumshauri atumie neno usaili badala ya udahili. *Dahala yaduhulu duhul* sasa hiyo naogopa.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Kilimo Kizimbani kimeshapatiwa usajili katika Baraza la Vyuo vya Ufundi Tanzania *(NACTE).* Hivyo, kinawajibika kufuata utaratibu mzima wa uendeshaji wa mafunzo kama ulivyoelekezwa na Baraza hilo. Moja kati ya taratibu hizo ni usaili wa wanafunzi. Katika mwaka wa masomo 2011/2012 chuo kilifanyia usaili wanafunzi 618 kati yao 262 walikuwa na sifa za chini za kuweza kujiunga na chuo. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo chuo kimechukua wanafunzi 86 tu ambao walianza masomo tangu tarehe 7 Novemba, 2011.

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Je, chuo chetu kinashirikishwa vipi katika upangaji wa mitaala.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Kilimo Kizimbani ni chuo cha kilimo ambacho kiko chini ya *NACTE*. Moja katika upembuzi yakinifu unaofanywa ni *NACTE* kuona kwamba mitaala yao imekaa vizuri na inakubalika na ndio wanawakubali. Kwa hivyo, wao wenyewe watu wa kilimo ndio wanaotengeneza hiyo mitaala na sio Wizara ya Elimu.

Nam. 76

Tatizo la Maji Pete

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Ni muda mrefu sasa usiopungua miaka 10 wananchi wa Pete hawana huduma ya maji safi na salama.

(a) Je, Mhe. Waziri tatizo hili la wananchi wa Pete analifahamu.
(b) Kama analifahamu ni hatua gani Serikali inazichukua au itazichukua katika kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi juu ya hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi wa Pete

wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia kianzio cha maji Unguja Ukuu hali ambayo miaka ya nyuma huduma hiyo haikuwa nzuri kwa kiasi. Lakini hata hivyo, kuanzia mwaka 2010/2011 tayari wananchi hao wananufaika na huduma hiyo muhimu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na juhudi mbali mbali za kuwapatia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama ikiwemo kijiji cha Pete. Miongoni mwa juhudi hizo ni zile za karibuni zilizofanywa kwa kushirikiana na Mhe. Mwakilishi wa Muyuni za kuyatoa maji kutoka katika visima vya Unguja Ukuu hadi Pete na kwa hivi sasa huduma hiyo inaendelea vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya rafiki yangu, mchapa kazi mwenye busara na mtarajiwa wa nafasi kubwa zaidi ya hiyo kutokana na utendaji wake makini na usikivu naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mhe. Naibu Waziri yanatofautiana na hali halisi ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo. Je, Mhe. Naibu Waziri kama kawaida yako utakuwa tayari kufuatana na mimi kupata ukweli wa tatizo hilo. Mhe. Mwenyekiti, swali (b) kwa kuwa mwakilishi wa jimbo hilo amekiri ameshatumia fedha nyingi mno kwa ajili ya wananchi hao lakini tatizo bado liko pale pale. Kwa vile ni rafiki yangu utakuwa tayari kunisaidia suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, swali (c) kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo shughuli zao kubwa ni kilimo. Je, huoni kukosekana kwa maji kunarudisha nyuma juhudi zao za uzalishaji kutokana na muda mwingi kutumia kusaka maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la

nyongeza kwanza naomba nimshukuru sana kwa kushirikiana na wizara yangu kwa kuwaondolea matatizo wananchi hususan tatizo la maji likiwemo na umeme. Nashukuru kwamba tunashirikiana kikamilifu juu ya hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba niko tayari kushirikiana nae kwa hali zote kama vile ambavyo tunashirikiana katika masuala mengine, ili kuondoa tatizo hili katika kijiji.

Nam. 77

Tatizo la Maji Jambiani Mfumbwi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Eneo la Jambiani Mfumbwi limekuwa ni eneo mojawapo muhimu kwa uchumi wa Zanzibar kutokana na ukuaji wa shughuli za kitalii katika maeneo ya Kusini Unguja. Hata hivyo, eneo hili linakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama.

Je, Mhe. Waziri, ni mikakati gani Serikali itaweka ili kuweza kuondoa tatizo hili na kuepusha kuzorota kwa shughuli za kitalii katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa eneo hilo wananufaika na huduma bora ya maji safi na salama kupitia mradi uliojengwa na

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Mamlaka ya Maji pamoja na nguvu za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa kilichotokea hivi karibuni ilikuwa ni kuungua pampu na kwa sasa Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tayari imeshaliondoa tatizo hilo na wananchi wa eneo hilo wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze tena Mhe. Naibu Waziri kwa mara nyengine ambaye ni Waziri mtarajiwa wa nafasi kubwa zaidi ya hiyo kwa mashirikiano mazuri aliyoonesha na kurudisha huduma ya maji kurudi katika jimbo hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua pampu za akiba ili kuondoa usumbufu kama uliojitokeza katika kijiji cha Jambiani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Mamlaka ya Maji inao mpango mkubwa wa kununua pampu nyingi sana za akiba na kwa sasa tumeshaanzia kufanya shughuli hizo na tayari pampu zipo katika ofisi yetu ya Mamlaka ya Maji.

Kwa hivyo, tatizo kama hilo la kuungua pampu basi wakati wowote mtakaotupa taarifa tutajitahidi kufuatilia na tutakufungieni pampu mpya kabisa.

Nam. 84

Ujenzi wa Barabara

Mhe. Mussa Ali Hassan – Alijibu:

Tunaipongeza Serikali kwa kuzifanyia matengenezo makubwa barabara mbali mbali za Unguja hususan barabara inayoelekea Fuoni. Hata hivyo, kumebainika kuwa katika maeneo mengi yanayojengwa barabara huwekwa *round about* na baada ya muda mfupi *round about* hizo huvunjwa kwa mfano eneo la Nyumba mbili – Mwanakwerekwe.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni sababu zipi zilizopelekea *round about* hizo kuvunjwa.

(b) Kwa kawaida kabla ya ujenzi kunakuwa na *plan* ya ujenzi inayojumuisha vipimo mbali mbali ikiwemo urefu na upana wa eneo linalojengwa. Je, Mhe. Waziri, katika Wizara yako wakati wa ujenzi wa barabara jambo hili huwa halifanyiki.

(c) Kwa kuwa katika Wizara kuna wataalam wa mambo ya barabara. Je, wakati wa matengenezo ya barabara huwa hawashirikishwi kutoa mawazo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, sababu zilizopelekea kuvunjwa kwa *round about* hiyo ni sababu za kiusalama baada ya kushindikana kuondoshwa kwa nyumba zilizokuwepo pembezoni mwa eneo la barabara ya kutoka Mwanakwerekwe hadi Nyumba mbili ili kuweza kukidhi ujenzi wa barabara hii.

(b) Mhe. Mwenyekiti, suala la mpango kazi wa ujenzi hujumuisha vipimo na huwa linafanyika kabla ya mradi wowote kuanza.

(c) Mhe. Mwenyekiti, wataalam wa Wizara yetu huwa wanashiriki kikamilifu katika miradi kama hiyo. Ushiriki wao huwa ni muhimu zaidi kwa maslahi ya Serikali na jamii kwa ujumla.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa gharama kubwa huwa inatumika wakati wa ujenzi wa barabara. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kufanya hivyo ni kutia hasara serikali ya kujenga na kubomoa kila wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika *disign* tulikuwa tuna dhamira hiyo ya kutengeneza round about, lakini kilichotukwaza, tungeweza kusema kwamba tunahitaji kutengemeza *round about* ingetulazimu tutafute fedha za kulipa fidia ya nyuma ili kuongeza eneo na kuzingatia kwamba fedha zenyewe zilizotumika ni miongoni mwa barabara tatu na kiasi cha fedha kilikuwa karibu bilioni 2. Tungeweza kusubiri kukidhi hiyo haja ya kutengeneza *round about* basi ingepelekea mradi huu kuchelewa na pengine kushindikana kufanya hivyo.

Napenda nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba barabara ile ujenzi uliojengwa, kama kutakuwa kuna haja basi baada ya kupatikana fedha za kuweza kutosha kuweza kuvunja nyumba na kutoa fidia, ndipo tutakuwa tuna haja ya kuongeza *round about* kwa mara ya pili. Lakini kwa muda huu nataka kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba hakukuwa na gharama yoyote ya ziada iliyotumika katika uondoshaji wa *round about* ile.

Nam. 36

Uhuru wa Vyombo vya Habari na Utawala Bora

Mhe. Farida Amour Mohammed (Kny: Mhe. Hamza Hassan Juma) – Aliuliza:-

Katika programu ya kuondosha umaskini hapa Zanzibar, serikali imeweka clasta tatu. Moja kati ya hizo ni utawala bora. Nchi yoyote yenye utawala bora na haki za binadamu basi ni lazima kuwe na uhuru mkubwa wa vyombo vya habari.

(a) Mhe. Waziri, unayo taarifa kwamba wadau wa vyombo vya habari wamefanya kazi kubwa ya kuleta mapendekezo ya mswada wa sheria ya vyombo vya habari, lakini ofisi yako imeukataa. Je, suala hilo ni kweli.

(b) Kama ni kweli, kuna tatizo gain hadi hii leo mswada huo bado haujaletwa hapa Barazani.

(c) Huoni kucheleweshwa mswada huu ni kudumaza uhuru wa vyombo vya habari.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo –Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuwaarifu wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba ni kweli kuwa serikali imeweka clasta tatu, moja kati ya hizo ni utawala bora. Nchi yoyote yenye utawala bora na haki za binadamu, ukweli ni kwamba wajibu wake, uhuru wa vyombo vya habari ambao utakuwa ukifuata sheria za nchi husika kama zinavyoitishwa na Mabunge au Baraza la Wawakilishi.
Pia uhuru huo lazima uwe na mipaka yake ili kila mtu apate haki yake ya kikatiba na sheria zilizowekwa kisheria na nchi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 36 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Swali la kwanza lilikuwa ni kwamba wizara imeukalia mswada huo. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wizara yangu ilipata mapendekezo ya mswada wa sheria wa kutoka kwa baadhi ya wadau wa vyombo vya habari na vile vile kutoka Baraza la Habari Tanzania (MCT), ambao pia uliwasilishwa katika semina ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hapo Mnazi Mmoja na kujadiliwa mswada huo na haukukaliwa wala haukupuuzwa.

(b) Ni tatizo gani hasa mpaka leo mswada haujaletwa. Mhe. Mwenyekiti, tatizo lipo, kwani baada ya hatua hiyo wizara yangu imebaini kwamba wadau wengi hawakupata fursa ya kuchangia mswada huo. Mfano wamiliki wa vyombo vya habari kutoka Unguja hawakupata nafasi hiyo ya kuuchangia. Lakini wadau wenyewe yaani wasikilizaji wa redio, wasomaji wa magazeti na kadhalika nao vile vile hawakupata fursa hiyo ya kuchangia, isipo waandishi wa habari wachache sana ndio walipata fursa hiyo. Kwa hivyo, tumeona kwamba haikuwa sahihi.

Aidha, waandishi wa habari kutoka Pemba wakiwa wachache mno walishirikishwa, lakini wamiliki wa vyombo vya habari na wadau wengine kutoka Pemba hawakushirikishwa kabisa. Jambo ambalo kwa kweli wadau hao waliosalia kutoka Pemba tumeona hawakutendea haki. Kwa hivyo, kwa taarifa tu ni kwamba sheria hii sio ya waandishi wa habari tu bali ni ya wamiliki wa vyombo vya habari na wadau

wengine wakiwemo hao wasikilizajiwa redio na wasomaji wa magazeti na kadhalika.

(c) Kuhusu kuchelewa kwa mswada huo huwenda ukadumaza uhuru wa vyombo vya habari. Mhe. Mwenyekiti, mimi naona mswada huu bado haujachelewa na wala haujadumaza uhuru wa vyombo vya habari, isipokuwa unataka kuharakishwa tu kutokana na umuhimu wake. Hata hivyo, wizara yangu tayari imeanza kuchukua hatua za utekelezaji wa suala hilo kwa kuwasiliana na Ofisi za UNDP hapa Zanzibar kwa kuandika mradi unaoitwa "*review of the news paper act of 1998 and capacity development of the department of the information service in Zanzibar".*

Mradi huu hivi sasa unatafutiwa fedha na umekabidhiwa UNESCO ambao ndio walioandika mradi huu wakishirikiana na Mkurugenzi wa Maelezo pamoja na maafisa wake. Jumla ya milioni 30 zitahitajika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba mswada huu ulikuwa haukukamilisha taratibu kwa sababu wadau wengi hawakushirikishwa na kwa kuwa mswada huu ni muhimu kwa vyombo vya habari na wakati umeshachelewa.

Je, Mhe. Waziri ni lini watawashirikisha wadau wote ili mswada huu uletwe wa kuvipauwezo vyombo vya habari viwe na sheria ambayo itakuwa inakidhi mahitaji yao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba bado

hatujachelewa. Tumeshatengeneza mradi, wameshakabidhiwa UNESCO na tunawasubiri wao wakati wowote watakapokabidhi hizo fedha basi tunaanza semina hiyo ili kuhakikisha kwamba wadau wote tuliowataja hapa, yaani washiriki kama wasikilizaji wa redio, wasomaji wa magazeti, waandishi wa habari na wamiliki wa vyombo vya habari wote washirikishwe. Ndio maana kwa nini hatujafanya hivyo, tukasema tusiulete kwanza mpaka huu mswada uchangiwe vya kutosha ili kila mdau ihakikishwe kwamba kuna *input* zake mule, isijekuwa imechukuliwa upande mmoja. Tulisema ni milioni 30 zitahitajika, tutakapozipata wakati wowote basi halani tutafanya hivyo. Ahsante sana.

KAULI ZA MAWAZIRI

Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Kipindi cha mwaka 2007/2008

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa lengo la kuwatumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2007/2008.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani za pekee nazitoa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi, Dk Ali Mohammed Shein, kwa busara na hekima kubwa alizonazo na anazozitumia katika kusimamia maendeleo ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwasilisha Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ya mwaka 2007/2008. Tume ya haki za binadamu ni chombo cha Muungano wa Tanzania. Hivyo, ripoti hii ya tume ya haki za binadamu na utawala bora, imeweka taarifa za shughuli za tume kwa Zanzibar katika sura ya nne ili kuleta urahisi wakati taarifa hii itakapowasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uimarishaji wa utawala bora na haki za binadamu hapa Zanzibar, lilipewa msukumo maalum hapo Novemba mwaka 2000, wakati Rais wa awamu ya sita Mhe. Aman Abeid Karume alipoanzisha Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora, iliyopewa jukumu la kusimamia masuala ya kikatiba na uimarishaji wa utawala bora na ukuzaji na utekelezaji wa misingi ya haki za binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni idara huru ya serikali inayojitegemea, iliyoundwa kwa mjibu wa ibara ya 129 mpaka 130 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyorekebishwa na mabadiliko ya 13 ya katiba yaliyofanyika mwaka 2000, pia sheria ya tume ya haki za binadamu na utawala bora nambari 7 ya mwaka 2001, kama ilivyorekebishwa na sheria nambari 16 ya mwaka 2001 ibara ya 130/6 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kifungu cha 3 cha sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nambari 7 ya mwaka 2001, imeipa mamlaka tume kufanya kazi Tanzania Bara na Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukidhi matakwa hayo, Baraza la Wawakilishi Zanzibar liliridhia sheria ya tume kwa kutunga sheria, yaani *extension act* ya tume ya haki za binadamu na utawala bora nambari 12 ya mwaka 2003, iliyofuatiwa na marekebisho ya sheria ya tume ya haki za binadamu na utawala bora nambari 7 ya mwaka 2001, yaliyofanywa na Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sheria ya *miscellaneous amendment* nambari 8 ya mwaka 2006. Kutokana na marekebisho hayo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba na Utawala Bora Zanzibar wakati huo, kupitia *legal notes* nambari 31 alitangaza uwamuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuridhia tume kufanya shughuli zake Zanzibar kuanzia tarehe 30/4/2007.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ya tume ya haki za binadamu na utawala bora ni ya aina yake, kwani inaonesha shughuli na changamoto za tume baada ya kuanzishwa na kuendelea kuonesha nafasi muhimu ya suala la haki za binadamu ambalo lilianzishwa katika tawala za zamani kama haki asili hadi kwenye azimio la umoja wa mataifa kuhusu haki za binadamu katika karne ya 20. Taarifa inaonesha pia masuala ya haki za binadamu na utawala bora ni ya msingi katika kuleta maendeleo endelevu, demokrasia na amani mahala popote duniani.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii ya mwaka 2007/2008 japo kwa muhtasari imejaribu kueleza shughuli za tume katika kutoa elimu kwa umma, kufanya uchunguzi na malalamiko ya wananchi, kufanya utafiti, kutoa ushauri wa kisheria, kukagua magereza na vituo vya polisi na kutoa mapendekezo kwa wizara na idara za serikali na wadau wengine. Shughuli zinazosaidia tume itekeleze wajibu wake kama vile za utawala na kuendeleza uhusiano wa wadau mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kupitishwa kwa sheria ya tume kufanya shughuli zake Zanzibar, ilikuwa ikipokea na kushughulikia malalamiko ambayo yanahusi wizara na idara za Muungano tu. Hadi kufikia Juni 30, 2008 Ofisi ya Tume Zanzibar ilikuwa imepokea jumla ya malalamiko 315, kati ya hayo malalamiko 103 sawa na asilimia 32.7 yalipokelewa katika mwaka 2007/2008. Idadi hii ni ndogo kutokana na ukweli kwamba tume ilianza kazi rasmi Zanzibar tarehe 30/4/2007.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 tume ilifanya ziara katika mikoa na wilaya za Zanzibar kwa madhumuni yafuatayo.

1. Kuitambulisha tume kwa viongozi mbali mbali wa serikali, vyama vya siasa, dini, jumuiya za kiraia na wananchi wote kwa ujumla, ili waifahamu na waweze kutumia na kunufaika na huduma zinazotolewa na tume.

2. Kutembelea na kukagua vituo vya polisi na vyuo vya mafunzo kwa lengo la kujua hali ya wafungwa na mahabusu, mazingira ya maeneo hayo, maslahi ya wafanyakazi ili kujionea kama haki za binadamu na misingi ya utawala bora inazingatiwa.

3. Kutoa elimu kwa umma kuhusu uelewa juu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa njia ya mikutano ya hadhara, katika mikoa, wilaya, taasisi za elimu na shehia mbali mbali za Zanzibar.

4. Kufanya utafiti na uchunguzi wa hadharani kuhusu utekelezaji wa haki za watoto Zanzibar.

Baada ya ziara hiyo tume ilibaini mambo ya jumla yafuatayo.

Elimu zaidi itolewe kwa askari ili waepukane na vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Serikali ishauriwe somo la haki za binadamu na utawala bora kwenye mtaala wa masomo shuleni, ili elimu hiyo iwafikie watoto mapema.

Ofisi za mikoa na wilaya ziandae maofisa maaluma watakaoshughulikia malalamiko yanayowasilishwa kutoka kwenye tume.

Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani, walilalamika kuwa viongozi wa serikali walichanganya utendaji wa vyombo vya serikali na siasa.

Aidha, malalamiko yaliyotolewa kwa vipindi vya chaguzi zilizopita, wananchi wasio na hatia walipigwa na askari wa vikosi.

Watuhumiwa walio katika vyuo vya mafunzo wanakosa haki ya huduma ya wakili au msaada wa kisheria.

Ulitolewa ushauri kuwa sheria inayohusu uteuzi wa masheha ifanyiwe marekebisho ili kuweka wazi vigezo vya uteuzi huo kwa lengo la kuhakikisha kuwa, wanaoteuliwa wana sifa na uwezo wa kufanyakazi hiyo ipasavyo.

Maeneo ya ardhi yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi maalum yakiwemo skuli, vituo vya polisi na vyuo vya mafunzo hayajatolewa hati milki, hivyo yapimwe rasmi na kutolewa hati ili kurahisisha udhibiti wake dhidi ya uvamizi wa wananchi.

Vijana wenye umri wa miaka 12 hadi 15 wanaotoroka skuli, serikali haijachukua hatua za kutosha kukabiliana na tatizo hilo.
Serikali ilishauriwa iangalie namna ya kuwasaidia watoto kupata haki yao ya elimu kwa kusaidia kugharamia elimu kwa watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuchangia elimu.

Viongozi pamoja na wananchi Pemba waliomba katiba zisambazwe kwa wananchi ili waisome na kujua haki zao.

Baadhi ya wananchi kukoseshwa haki ya kupiga kura kwa kutawanywa, kufukuzwa kwenye maeneo ya vituo vya kupiga

kura wakati serikali inahamasisha wananchi juu ya haki ya kupiga kura kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo ya tume kuhusu Jeshi la Polisi. Serikali zishughulikie fidia zinazohusu ili askari anapoumia akiwa kazini alipwe fidia. Haki ya likizo ya uzazi na haki ya likizo ya mwaka kwa askari, iangaliwe upya ili isipingane na misingi ya haki za wafanyakazi.

Mikataba ya kiinua mgongo na pencheni ya askari polisi iangaliwe upya ili kuondoa manung'uniko.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na jeshi la polisi, waangalie upya suala la matibabu ya mahabusu. Wizara ya Mambo ya Ndani iweke mikakati ya kuwapatia askari nyumba zenye hadhi ya kifamilia na za kutosha. Wizara ya Mambo ya Ndani iimarishe hali na miundombinu ya vituo vya polisi na kuwapatia vitendea kazi.

Jeshi la polisi lijenge vituo vya polisi vya kisasa katika maeneo yenye upungufu wa vituo. Jeshi la polisi litenge fedha katika bajeti yake kwa ajili ya kutengeneza majengo yaliyochakaa na kujenga vituo vipya katika maeneo yenye vituo vibovu visivyofaa. Jeshi la Polisi na taasisi mbali mbali za serikali ikiwemo, Wizara ya Katiba na Utawala Bora ya wakati huu, kwa sasa ni Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tume ya uchaguzi na asasi zisizo za serikali zitowe elimu ya haki za binadamu na wajibu kwa umma.

Mhe. Mwenyekiti, tume imefanya mapendekezo ya mipaka ya kazi baina ya vyuo vya mafunzo na Jeshi la Polisi, iheshimiwe ili kupunguza malalamiko dhidi ya askari polisi na kuhakikisha kwamba wanaacha kuwatesa watuhumiwa walioko vyuo vya mafunzo. Uongozi wa Chuo cha Mafunzo kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi, ichukuwe hatua ya kutenganisha mahabusu, wanafunzi watoto na watu wazima vyuoni.

Mhe. Mwenyekiti, uandaliwe utaratibu wa kuharakisha upelelezi na uendeshaji wa kesi pamoja na utekelezaji wa haki ya burudani kwa wanafunzi na mahabusu uimarishwe zaidi. Hali ya chakula katika vyuo vya mafunzo ifanywe iwe bora zaidi, kwa kuwapatia mboga za majani, matunda, sukari, nyama na maharagwe yawekwe mafuta. Pia hatua zichukuliwe kujenga vyuo ndani ya vyuo vya mafunzo, yaani kujenga vyuo vya Kuran ndani ya vyuo vya mafunzo na matumizi ya mitondoo katika vyuo yapigwe marufuku.

Sare za askari wa vyuo vya mafunzo zifanywe ziwe bora zaidi na huduma za afya katika vyuo vya mafunzo ziangaliwe upya. Wanafunzi wanaohamishwa kutoka chuo kimoja kwenda kingine wapewe mapema vielelezo au kumbukumbu za kesi zao. Askari polisi na askari wa vyuo vya mafunzo washirikiane kufuatilia malalamiko kwa baadhi ya askari hawarejeshi vitu vinavyotolewa kama dhamana na mahabusu.

Vile vile wanafunzi wapewe haki ya huduma ya msaada wa kisheria kwa mujibu wa taratibu. Iwekwe huduma maalum ya afya kwa wagonjwa wa ukimwi katika vyuo vya mafunzo na wanafunzi wenye maradhi ya kuambukiza watengwe ili wasiwaambukize wengine.

Mhe. Mwenyekiti, askari wa vyuo vya Mafunzo wajengewe nyumba za makaazi zinazokidhi mahitaji na pia serikali ichukuwe hatua kuvikarabati vyuo vya mafunzo viliopo. Maslahi ya askari wa vyuo vya mafunzo yafanywe yawe bora zaidi na wawekewe utaratibu kuhakikisha kuwa wanalipwa maslahi yao kwa wakati. Vyuo vya Mafunzo vipewe nyenzo za kufanyia kazi kama vile magari na kadhalika. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iongeze bajeti kwa vyuo vya mafunzo ili viweze kuboresha huduma zake.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo ya tume kuhusu utekelezaji wa haki za watoto. Taasisi za serikali na zisizo za kiserikali, ziongeze jitihada za kuwahimiza wazazi na walezi kutowatelekeza watoto na kuwalea kwa kuzingatia maadili mema. Serikali iendelee kushirikiana na asasi mbali mbali katika kuwalinda na kuwaendeleza watoto wanaoishi mitaani, yatima na wanaishi katika mazingira magumu. Watoto wapewe fursa zaidi ya kutoa mawazo na hisia zao kuwa ni haki yao kushiriki katika masuala yanayowahusu. Walimu na wazazi washirikishwe kwa karibu zaidi katika kupanga maendeleo ya elimu ya watoto. Wazazi, walezi na walimu watowe adhabu ambazo hazivunji sheria. Vyomb vya dola viongeze kasi ya kushughulikia kesi zinazohusu watoto.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na wadau wengine wa haki za watoto, waongeze jitihada kupiga vita ajira mbaya kwa watoto. Watoto wasitumike kuendesha biashara. Kuundwe kamati za watoto katika ngazi za shehia, wilaya na mikoa. Mahakama na polisi viimarishwe ili kuanzisha vitengo vya kushughulikia kesi za watoto, kuwepo na mpango thabiti wa kuwapatia madawati watoto shuleni.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena natoa shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kushirikiana na mimi katika kutekeleza majukumu ya wizara yangu.
Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba baada ya kupokelewa rasmi ripoti hii, wataifanyia kazi ripoti hii na kuleta taarifa zao kwenye kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA YA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR KUHUSU TAARIFA YA WAZIRI JUU YA TAARIFA YA MWAKA 2007/2008 YA HAKI ZA BINAADAMU NA UTAWALA BORA KWA UPANDE WA ZANZIBAR.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuchukuwa fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana asubuhi hii ya leo, ili niwasilishe rasmi kwa niaba ya Mwenyekiti, maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya Taarifa ya Waziri, kuhusu Taarifa ya mwaka 2007/2008 ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia, kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nisiache kuendelea kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mji Mkongwe, walionipa heshima ya kuingia katika chombo hiki na kufanya kazi yao waliyonituma.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haji Omar Kheir kwa kuwasilisha mbele ya Baraza, taarifa hii muhimu kama Sheria inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tukiisubiri sana taarifa hii kwani itatuwezesha kujua wapi tulipotoka, wapi tulipo na wapi tunaelekea katika misingi ya haki za binaadamu na utawala bora Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mpungufu wa fadhila nisipowapongeza na kuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora kwa upande wa Zanzibar, kwa mashirikiano yao ya dhati waliyotupa wakati Kamati yetu ilipofanya ziara kwenye Afisi yao hapo Mazizini mnamo mwezi wa Disemba, 2011.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina jumla ya Wajumbe saba na makatibu wawili. Kwa hivyo, naomba kuwashukuru na kuwapongezi kwa dhati kwa mashirikiano yao wanayotupatia na nawaomba wazidishe mashirikiano miongoni mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwatambua Wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Abdalla Ali - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan - Mjumbe
5. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Mjumbe
6. Mhe. Suleiman Hemed Khamis- Mjumbe
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
9. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu.

(Makofi)

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza serikali kwa jitihada zake kubwa ilizozichukua na kuhakikisha kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inafanya kazi zake Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa masuala ya Haki za Binadamu ndio yanayopigiwa kelele duniani kote na tunaona mifano ya nchi mbali mbali za Afrika

Kaskazini na Mashariki ya Kati katika kipindi hiki, jinsi wananchi wanavyozigombania na kuzidai haki hizo.

Kitendo cha kijana mfanya biashara ya matunda na mboga mboga wa Tunisia aitwaye Bouazizi kuchoshwa na maonevu na bughudha za askari wa Manispaa ya Jiji la Tunis na kuamua kuoneshwa kuchukizwa kwake kwa kujichoma moto hadharani mbele ya jengo la Manispaa hiyo.

Kwa kweli kilitosha kuchochea vuguvugu la kudai mabadiliko ya kisiasa yanayotaka kuheshimiwa kwa misingi ya haki za binadamu na utawala bora katika nchi hizo za Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati. Mfano huo unatupa fundisho la kutosha juu ya umuhimu wa kutekeleza haki za binadamu na utawala bora katika nchi zetu pia.

Mhe. Mwenyekiti, Taarifa ya Tume kuhusu Zanzibar inapatikana ukurasa wa 98 – 163 ya ripoti. Taarifa hiyo inatueleza kuwa kuanzia mwaka 2001 hadi Juni 2008 imepokea malalamiko 315 kwa upande wa Zanzibar. Takwimu hizi zinadhihirisha wazi kuwa wananchi wanaitumia Taasisi hii ipasavyo.

Hata hivyo, tunaiomba Tume hii izidi kujitangaza ili wananchi waweze kuitambua kwa kina na kuweza kujua ni sehemu au Taasisi gani inayoweza kuwasaidia endapo haki zao zitavunjwa. Sambamba na hilo kwa kutumia njia mbali mbali izidi kuielimisha jamii juu ya haki zao na misingi ya utawala bora. Kwani imebainika kuwa baadhi ya wananchi hususan wa vijijini bado hawayaelewi masuala haya muhimu kama taarifa yenyewe ya Tume ilivyokiri.
Mhe. Mwenyekiti, tunaunga mkono taarifa iliyotolewa na Tume hii kwenye kifungu cha 4.4. kuhusiana na kutembelea na kukagua Vituo vya Polisi na Vyuo vya Mafunzo. Hii ni kutokana na kuwa mambo haya yaliyoelezwa kwenye kifungu hiki tumeyashuhudia

wenyewe wakati Kamati yetu kulipotembelea na kukagua Vyuo vya Mafunzo – Zanzibar mnamo mwezi wa Disemba, 2011.

Mhe. Mwenyekiti, tulivitembelea Vyuo vya Mafunzo kwa kuwa tunalo jukumu la kusimamia masuala ya Utawala Bora kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala haikuridhishwa kabisa na namna wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo, mahabusu pamoja na Askari wa Mafunzo wanavyohudumiwa.

Hivyo, Kamati yetu inaiomba serikali kuyazingatia na kuyachukulia hatua mapendekezo ya Tume hii kama yalivyoelezwa, ili kujenga mustakbali mzuri wa nchi yetu. Kwani si jambo la busara na la kupendeza la kuona zinatolewa taarifa hizo hizo kila mwaka huku kukiwa hakuna utekelezaji au hatua zozote zinazochukuliwa na serikali kurekebisha hali hiyo.

Mara nyingi Waheshimiwa Wawakilishi ndani ya Baraza hili wameelezea kuchoshwa na kauli zenye maneno matamu na ahadi nyingi za kushughulikia maeneo mbali mbali yanayolalamikiwa, lakini bado hatua hazichukuliwi na pale zinapochukuliwa huwa ni kwa kiwango cha chini kiasi kwamba huwa haziondoi kiini cha matatizo yanayolalamikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inasisitiza haja ya kuangalia mapendekezo yote ya Tume kuhusu malazi, msongamano wa wanafunzi na mahabusu kwenye Vyuo vya Mafunzo, kujengwa vyoo na kuachana na kutumia mitondoo, sare za wanafunzi, chakula, haki ya kuabudu, haki ya mawasiliano, burudani, usafiri, nishati, huduma za afya, ukatili dhidi ya wanafunzi, na hali ya kuchanganya watoto na mahabusu na wafungwa wengine. Hayo ni kwa wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo.

Kwa upande mwengine, serikali pia ichukue hatua madhubuti katika kukabilina na matatizo ya Askari Polisi na Askari wa Vyuo vya Mafunzo yaliyoainishwa yakiwemo sare za askari, makaazi ya askari, vitendea kazi hasa usafiri, na ustawi wao ikiwa ni pamoja na mishahara, likizo na masomo. Kamati inaitaka serikali kuyaangalia kwa makini mapendekezo ya hatua za muda mfupi na za muda mrefu katika kuyapatia ufumbuzi matatizo haya kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 116 na 117 wa Ripoti ya Tume.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu pia inaitaka serikali kuyaangalia kwa kina na kuyafanyia kazi malalamiko na maoni yaliyotolewa na wananchi pale Tume ilipokutana nao na ambayo yameorodheshwa kwenye Taarifa ya Tume ukurasa wa 105 – 108, ambayo nafurahi kwamba Mhe. Waziri naye ameyanukuu katika taarifa yake aliyoitoa mbele ya Baraza lako hivi punde. Ijapokuwa yote ni muhimu Mhe. Mwenyekiti, tunasisitiza zaidi serikali kuyachukulia hatua maeneo yafuatayo yaliyotajwa kwenye sehemu hiyo:-

1. Pendekezo la kuingiza katika mitaala ya maskuli somo la Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kifungu (g) kilichopo ukurasa wa 106.

2. Migogoro ya ardhi kati ya kati ya wananchi na wawekezaji na pia kati ya wananchi na baadhi ya viongozi na watendaji serikalini. Kifungu (l) kilichopo ukurasa wa 106.

3. Malalamiko kuhusu askari wa Vikosi vya SMZ kuingilia kazi za Polisi na kuwanyanyasa raia. Kifungu (m) kilichopo ukurasa wa 106.
4. Rushwa katika Mahakama hasa kwa baadhi ya Mahakimu, ambako kunapelekea kuathiri utoaji wa haki na kukosekana uadilifu katika kushughulikia kesi. Kifungu (p) kilichopo ukurasa wa 107.

5. Haja ya sifa zinazotumika katika uteuzi wa Masheha kuwekwa wazi. Kifungu (s) kilichopo ukurasa wa 107. Mhe. Mwenyekiti, pengine wakati sasa umefika wa kuja na utaratibu wa Masheha kuchaguliwa na wakaazi wa Shehia badala ya kuteuliwa, ili wawajibike zaidi kwa wanaowatumikia.

6. Wananchi kukoseshwa haki ya kupiga kura, wakati serikali inahamasisha wananchi juu ya haki ya kupiga kura kupitia vyombo vya habari. Kifungu (x) kilichopo ukurasa wa 108.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inaitaka serikali hususan Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyomo kwenye ukurasa wa 161 – 163 kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa, ili kulinda haki za watoto na kupambana na utumikishwaji wa watoto.

Miongoni mwa mambo hayo ni watoto na hasa wanafunzi kutumiwa katika mikutano ya kisiasa, watoto kuathirika na dawa za kulevya, kuwanyanyapaa watoto wenye ulemavu na kuhakikisha haki ya kupata elimu haiathiriwi na mambo mengine katika familia na jamii.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo hayo makhsusi, tunaiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuibana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuitengea fedha Ofisi ya Tume liyopo Zanzibar kwa ajili kuipa msukumo zaidi katika kutekeleza majukumu yake. Tunaliomba hili kwa kuwa bajeti inayotengwa kwa Tume haikidhi haja kutokana na majukumu mazito inayoikabili.

Mhe. Mwenyekiti, haipendezi kwa Serikali ya Muungano kuanzisha Taasisi na kuzipa mamlaka ya kufanya kazi Zanzibar, halafu ikaacha kuzihudumia na hivyo kuzifanya ziwepo kwa majengo tu na kushindwa kutoa huduma zilizokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo Kamati yetu inapendekeza ni kwa serikali kupitia waziri husika kuharakisha utungaji wa Kanuni, ili Tume iweze kufanya kazi kwa ufanisi hasa ukizingatia kuwa hii ni miongoni mwa Taasisi za Serikali na ina majukumu mazito kwa wananchi na serikali kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa Tume ijenge uhusiano mkubwa na Ofisi zote za Serikali pamoja na zisizo za Kiserikali, ili viongozi wa Taasisi hizo waelewe wajibu wao kwa watumishi wanaozitumikia ofisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa mara nyengine tena kwa kunipa nafasi hii pamoja na kunivumilia kuutumia muda wako adhimu, katika kuwasilisha maoni ya Kamati juu ya taarifa ya Waziri kuhusu Taarifa ya mwaka 2007/2008 ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora. Ni matumaini yetu kuwa mapendekezo ya Kamati, Tume pamoja na yale yatakayotokana na maswali ya Waheshimiwa Wajumbe, yatachukuliwa hatua kama tulivyopendekeza.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza kwa ustahamilivu na usikivu wenu kwa kipindi chote ambacho nikiwasilisha maoni ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa kwa kuwa tunalo jambo jengine mbele yetu, yaani semina na huu ni wakati wa kuuliza maswali. Lakini naomba maswali yetu yawe mafupi

kidogo, ili tumpe nafasi Mhe. Waziri aweze kujumuisha. Kwa hivyo, tuanze na maswali.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nami kwanza nianze kwa kuipongeza serikali, kwani itakuwa si vyema kwa hatua yake hii ya kukubali kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kwa hivyo, pongezi zangu ziende kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuunda chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa chombo hiki ndicho kioo, kwa sababu binadamu anapofanya mambo bila ya kujiwekea kioo, basi hawezi kujijua yuko katika hali gani. Kwa hivyo, tume hii ndio itakayokuwa ni kioo cha serikali kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo taasisi yenyewe kwamba inaitwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Naomba kupendekeza Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ni neno ambalo linachukua mambo mawili itakuwa haina maana hata kidogo kama hakukutolewa elimu pana na ya kutosha ikiwa wananchi hawajui maana ya tume hii.

Kwa kweli neno la Haki za Binadamu ni Elimu, sasa ikiwa tume hii na ipo kwa ajili ya wananchi, basi ni lazima wananchi wenyewe wazijue hizo Haki za Binadamu ni haki za aina gani, kwani bila ya wao kujua hii ni haki ya binadamu, nadhani hawawezi kujitokeza na kwenda kutoa maoni au kueleza chochote mbele ya tume.

Vile vile tunalo suala la Utawala Bora. Sehemu kubwa ya Ripoti ya Tume hii imegusia suala zima la Haki za Binadamu, sehemu ndogo sana iliyozungumzia kuhusiana na masuala ya utawala bora, kwa sababu utawala bora kama alivyoeleza Mhe. Mwenyekiti ni mambo mambo ya utawala wa sheria, uwajibikaji

wa serikali yenyewe, namna ya matumizi mazuri ya fedha za umma pamoja na rasilimali za nchi.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema tume ikajikita katika kuziangalia serikali namna gani zinatekeleza katika eneo hii, kwa sababu eneo la utawala bora liko katika upande wa serikali.

Kwa msingi huo basi Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri. Je, amejipanga vipi kwa sababu wizara yake ndio mratibu, kwani wizara yake ni wizara mtambuka katika suala hili. Kwa kuwa mapendekezo mengi yaliyotolewa utekelezaji wake unakwenda katika wizara pamoja na idara tofauti.

Hivyo, yeye ikiwa ndiye mratibu wa suala hili amejipanga vipi kuhakikisha kwamba anazisimamia wizara nyengine katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, kwa vyovyote vile ni mambo yanayohitaji masuala ya kibajeti pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri wizara yake kama mratibu imejiandaa vipi katika kuona utekelezaji wa ripoti hii unafanyika kwa ufanisi kama ambavyo imependekezwa na ripoti?

Swali langu jengine kwa kuwa ripoti imeshatolewa hii na inavyoonekana ni kwamba kila mwaka tume inatoa ripoti ya aina hii. Sasa si vizuri kuwa kila mwaka sisi tunasomewa ripoti tu, yaani kazi yetu ni kupokea ripoti tu, basi lazima tufike pahala tunapokea ripoti na baadaye ripoti inafanyiwa kazi kwa utekelezaji. Lakini jambo la msingi chombo hiki ni vipi tutafanya tathmini katika kuona ni namna gani hizi ripoti zimetekelezwa.

Kwa hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba wizara yake imeandaa utaratibu gani wa kufanya tathmini wa chombo hiki cha wananchi, ili tuone kwamba utekelezaji katika ripoti ya mwaka

uliopita imetekelezwa kwa kiwango fulani na tunahitaji tufanye nini, ili tuweze kwenda mbele katika hilo?

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri kuhusu suala la Haki za Binadamu. Mhe. Mwenyekiti, ripoti imetolewa kama alivyosema mwenzangu na tunashukuru sana Tume hii kwa kutoa ripoti zake, hivi sasa ripoti hii imesomwa kwa ajili ya utekelezaji.

Lakini na mimi niungane na mwenzangu kwamba kusomewa ripoti sio mwisho wake, isipokuwa mwisho wake ni ripoti kusomwa na yale maagizo au mapendekezo yanayotolewa na tume yakafanyiwa kazi.

Kwa hivyo, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kwa sababu tume imesema kwamba moja walililoligundua kuna wao ambao walikoseshwa haki zao za kupiga kura na hivi sasa ripoti imetolewa.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri wizara yake imejipanga vipi kuhusu kuyafanyia kazi kwa wale wananchi ambao walikuwa na haki ya kupiga kura na walikoseshwa kupiga kura, wakati ni haki yao ya msingi, ili mara nyengine wananchi wale waweze kupiga kura yao, kwa sababu ni haki yao ya Kikatiba ya msingi tena ni ya kibinadamu? Hilo ni moja.

Pili kama mapendekezo ya tume ilivyosema kwamba suala jengine walililoliona ni kuwa hivi sasa umefika wakati wa kuona Masheha wafanyiwe mapendekezo, ili uteuzi wao uwe mzuri na ikiwezekana iwe ni kuchaguliwa. Je, pamoja na hilo Mhe. Waziri atalishughulikia vipi suala hili kuona kama hivi sasa umefika wakati Masheha kuchaguliwa na wananchi na sio kuteuliwa kama wanavyofanyiwa hivi sasa?

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda kwenye swali moja kwa moja. Kwa kuwa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ni Haki ya Mzanzibari katika shughuli moja wapo ni ya uchaguzi.

Lakini kuna haki nyingi anazikosa ikiwemo huduma nyingi zinazotolewa hivi sasa nchini, kama vile huduma za benki, ajira, kutambulikana. Sasa kuna vijana wetu wanaojishughulisha na biashara kwende Kenya, basi pia kinatambulika na kinawapa fursa ya kufanya biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri Haki hii ya Binadamu ni lini serikali itazinduka iwape?

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami nataka kuuliza swali kuhusu ripoti hii. Kwa kweli ripoti hii inahusu Haki za Binadamu na kwa kiasi fulani mara nyingi haki inakiukwa, kwa hivyo mwanadamu huwa anadhalilishwa kwa haki yake.

Kwa mfano, mimi mwenyewe binafsi nimeshuhudia mara nyingi watuhumiwa wa makosa fulani hupelekwa Mahakamani ikiwa wamepigwa pingu tena mikono nyuma, kwa kweli hali ile ni kuvunja Haki za Binadamu na kumdhalilisha. Je, serikali itachukua hatua za aina gani kukomesha vitendo vya aina hii?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru tena kwa mara nyengine kunipa fursa hii ya kuweza kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maswali ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Kwanza nataka nichukue nafasi hii tena kumshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kutoa maoni ya kamati kufuatia Ripoti hii

ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba nimeyapokea maoni ya kamati yaliyotolewa, pia niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwa sababu Ripoti hii ni ya mwaka 2007/2008, basi baadhi ya mambo mengi sana tayari yameshachukuliwa hatua. Lakini kwa yale ambayo bado hayajachukuliwa hatua ninayapokea. Vile vile ushauri zaidi tutaupokea pale ambapo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala baada ya Baraza hili lako tukufu kuipokea rasmi ripoti hii na kwenda kuifanyiakazi. Kwa hivyo, mapendekezo ya kamati wizara yangu inayapokea na itahakikisha inayafanyiakazi hasa lile la utungwaji wa kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa wanne wameuliza maswali kwa hiyo naomba niende kwa Mhe. Mjumbe mmoja mmoja.

Kwanza alikuwa ni Mhe. Omar Ali Shehe, yeye alikuwa akizungumzia kuhusu suala la kutoa taaluma kwa wananchi juu ya suala hili zima la Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa wizara yangu imejipanga katika kutekeleza jambo hili kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, pia kupitia Idara ya Utawala Bora Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba mpaka wizara yangu inaundwa ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tulikuwa hatuna Sera ya Utawala Bora. Kwa hivyo, hivi sasa tayari tumeshaweka Sera ya Utawala Bora na imeshapitishwa rasmi na serikali. Kwa hiyo, yale yote ambayo yamo kwenye sera, basi tutajitahidi kuyafanyiakazi kama ilivyoagiza sera.

Kwa kweli wizara yangu imejipanga vizuri katika kufanya zoezi la Kutoa elimu kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wajumbe watakuwa

wameangalia *ZBC- TV* katika kipindi cha karibuni, yaani wiki chache zilizopita. Kutokana na hali hiyo, napenda nimpongeze sana Mkurugenzi wangu wa Utawala Bora kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, Mkurugenzi wangu ni mwanamama na wanamama wanakuwa wanafanyakazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imejipanga vipi katika suala zima la uwajibikaji wa serikali, yaani suala zima la utawala bora. Kwa kweli kama nilivyosema ni kwamba hivi juzi wiki iliyopita nilizingua rasmi Kamati ya Kitaifa ya Utawala Bora, ambayo inawashirikisha Wakurugenzi Mipango na Sera wa Wizara zote za Serikali pamoja na Taasisi Zisizo za Kiserikali vikiwemo Vyama vya Hiari kama vile Jumuia za Wafanyakazi, Chama cha Wanasheria pamoja na Taasisi nyengine za Kiraia.

Wajumbe hao ndio wanaunda Kamati hii ya Kitaifa ya Usimamizi wa Utawala Bora ikiongozwa na Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndiye Mwenyekiti wake. *(Makofi)*

Kamati hii ni ya kitaifa, lakini kila wizara au taasisi inatakiwa inatakiwa iwe na kamati hii, ili kamati hii iwe inapokea ripoti kutoka taarifa za wizara na taasisi moja moja. Kwa mujibu wa taratibu taarifa zile nitalazimika kuziwasilisha kwenye chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Wizara yangu imejipanga katika kufanya tathmini. Mhe. Mwenyekiti, ndio imejipanga na ndio maana nimesema kwamba tutapokea ripoti kutoka taasisi moja moja na taasisi za kiraia, lakini ile Kamati ya Kitaifa itawasilisha ripoti ile kwangu na hatimaye nitaiwasilisha kwenye Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, mtiririko huo ni uthibitisho kwamba tathmini ya kutosha itakuwepo.

Mhe. Subeit Khamis Faki na yeye alizungumzia kuhusu watu waliokoseshwa haki ya kupiga kura juu ya utaratibu wa kuwapatia haki zao. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, unajua

utata ni kwamba suala hili ni la muda mrefu, yaani ripoti hii ni ya nyuma. Lakini tabaan wale ambao walikoseshwa haki kwa kutumia taratibu zilizopo za kisheria, basi watakuwa wamechukua hatua ya kwenda kuripoti kwenye vyombo vinavyohusika na malalamiko yao yatakuwa yamepatiwa ufumbuzi kwa wakati ule.

Sasa kama watatokezea wengine ambao wamekoseshwa haki hiyo, basi nadhani taratibu zilizopo zitatumika katika kuhakikisha kuwa haki zao wanazipata. Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu suala la kuwapata Masheha kwamba maoni ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati pamoja na maoni ya Waheshimiwa Wajumbe, kwamba suala hili la namna ya kuwapata Masheha inaonelewa ni vizuri zaidi wakapatikana kwa njia ya kupiga kura.

Kwa kweli suala hapa ni sheria, kwa sababu hivi sasa Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imo katika kupitia Sera ya Madaraka Mikoani. Sera hii itaelekeza namna ya kufanya marekebisho katika sheria.

Sasa sheria wakati huo ikileta, yaani matakwa ya sheria yakihitaji kuwa watu hawa wachaguliwe, basi serikali hii ni sikivu na wala haina tatizo. Lakini kwa sheria ya sasa inasema Masheha wateuliwe. Kwa hivyo, hapa kuna tatizo la kisheria, sheria itakavyoamuliwa na Baraza hili kufanyika kutokana na mapendekezo ambayo yatapelekwa serikalini, ndivyo ambavyo serikali itatekeleza jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa sababu jambo hili linahitaji masuala ya kisheria, basi ni vizuri tukasubiri utaratibu wa kisheria ukamilike, ili jambo hilo liweze kutekelezeka. *(Makofi)*
Mhe. Rashid Seif Suleiman na yeye alizungumzia kuhusu Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi serikali kuzinduka. Mhe. Mwenyekiti, serikali imezinduka zamani sana kwamba haki ya

Mzanzibari ni kuwa na *ZID*. Kwa hivyo, suala hili nalo mkondo wake ni ule ule, kama yupo mtu ambaye anahisi hajapata na anastahili kupata *ZID*, basi nadhani njia ya msingi ni kufuata taratibu zilizopo, ili aweze kupatiwa *ZID* kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri tuendelee kuwaelimisha watu wetu na yule ambaye anayo haki na wala hakuna sababu kwa Mzanzibari mwenye haki alalamikie jambo hili, kama hatendewi haki basi nadhani afuate utaratibu uliopo, ili aweze kupata suala hili la *ZID*. Kwa kweli serikali imezinduka na ndio maana ikaanzisha kitu hiki.

Mhe. Mohammed Haji Khalid na yeye alizungumzia kuhusu suala la watuhumiwa kutiwa pingu ah! Mimi si mtaalamu wa masuala ya Kipolisi. Lakini ninavyojua mimi ni kwamba kuna njia nyingi za kumuongoza mtuhumiwa.

Njia ya kwanza ni kumuongoza kwa njia ya kawaida hasa pale mtuhumiwa ametii sheria, kwanza askari anakwenda na kuonesha kitambulisho chake kwamba hivi sasa nakuweka chini ya ulinzi na mtuhumiwa yule akafuata utaratibu na wala asilete tabu. Kwa hivyo, huyo mtuhumiwa hana haja ya kufungwa pingu na ataongozwa kwa utaratibu wa kawaida mpaka atafikishwa pahala panapohusika kulingana na *stage*, ikiwa Kituo cha Polisi au *stage* ya kufikishwa Mahakamani ama *stage* ya kufikishwa Mahabusu.

Lakini askari amewekewa mazingira ya kuweza kutekeleza wajibu wake, kama mtuhumiwa ataonekana anazo dalili za kutokuwa kuwa muaminifu kama ataongozwa kwa njia za kawaida za kibinadamu anaweza kuzikiuka kutokana na kumbukumbu zake za nyuma, basi huyo askari atalazimika kumpiga pingu. Vile vile ikiwa mtu huyo ataanza kuonesha dalili za kuleta fugo, nadhani taratibu hizi zimewekwa.

Mhe. Mwenyekiti, sipingani na Wanaharakati wa Haki za Binadamu, lakini ni jambo ambalo hao walioliweka wameliweka kwa misingi ya kuweza kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi hizi. Kwa hivyo, itakapofika pahala suala la kutia pingu linaonekana halistahili kabisa, basi serikali hii kama nilivyosema ni sikivu tutatoa maelekezo hayo kwa askari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa nadhani tuendelee kuliacha, lakini hatupendelei sisi kama serikali kutaka askari wetu atumie nguvu hata kidogo. Kwa kweli kuna mwahala hutakiwi kabisa kutumia nguvu, isipokuwa utumie diplomasia ya hali ya juu kumrai yule mhalifu, ili afuate vile unavyotaka wewe, yaani mpaka kufika pahala kutumia nguvu maana yake labda kutakuwa na jambo jengine ambalo limemsababisha yule askari aweze kutumia nguvu.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wameniuliza maswali haya pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wako wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza katika kujibu maswali haya.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaoafikiri ripoti hii ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kufanyika leo sasa zimekamilika.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sana kwa leo kufikia hapa ndio tumemaliza shughuli zetu za Baraza na tukijaaliwa tutaonana kesho tarehe 26/01/2012 saa 3:00 asubuhi.

Baada ya hapo nawanaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kama tulivyopewa taarifa ya semina tufike katika eneo la semina ambapo ni *Fishermen Resort*. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote tukitoka hapa moja kwa moja tuelekee huko. Ahsante sana.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/01/2012 saa 3:00 asubuhi)